BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA WA MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A (GATCE) 2019

## 634 STADI ZA KAZI

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA UALIMU DARAJA LA A (GATCE), 2019

# 634 STADI ZA KAZI

*Kimechapishwa na:*
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P 2624,
Dar es salaam, Tanzania.

**© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2019**

Haki zote zimehifadhiwa.

# YALIYOMO


DIBAJI .................... IV
1.0 UTANGULIZI .................... 1
2.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA SWALI 2
2.1 SEHEMU A .................... 2
2.1.1 Swali la 1: Usanii wa Picha, Chapa, Maumbo na Mapambo .................... 2
2.1.2 Swali la 2: Upimaji .................... 4
2.1.3 Swali la 3: Ususi .................... 6
2.1.4 Swali la 4: Maandalizi ya Ufundishaji .................... 8
2.1.5 Swali la 5: Muziki .................... 10
2.1.6 Swali la 6: Ufundishaji .................... 13
2.1.7 Swali la 7: Upishi .................... 15
2.1.8 Swali la 8: Ufundishaji .................... 17
2.1.9 Swali la 9: Usanii wa Picha, Chapa, Maumbo na Mapambo .................... 20
2.1.10 Swali la 10: Ufundishaji .................... 22
2.2 SEHEMU B .................... 25
2.2.1 Swali la 11: Sanaa za Maonyesho .................... 25
2.2.2 Swali la 12: Ushoni wa Nguo .................... 30
2.2.3 Swali la 13: Kilimo, Ufugaji na Uvuvi .................... 34
2.3 SEHEMU C .................... 37
2.3.1 Swali la 14: Misingi ya Kufundishia Somo la Stadi za Kazi .................... 38
2.3.2 Swali la 15: Upimaji .................... 41
2.3.3 Swali la 16: Maandalizi ya Ufundishaji .................... 45
3.0 UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA KUFAULU KWA WATAHINIWA KATIKA MADA .................... 47
4.0 HITIMISHO .................... 48
5.0 MAPENDEKEZO .................... 49
Kiambatisho A .................... 51
Kiambatisho B .................... 52

## DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania linayo furaha kutoa taarifa ya uchambuzi wa majibu ya watahiniwa wa Mtihani wa Kuhitimu Ualimu Daraja la A kwa somo la Stadi za Kazi. Taarifa hii imeandaliwa ili kutoa mrejesho kwa wanachuo, wakufunzi, waandaa sera, wadau wa elimu na jamii kwa ujumla jinsi watahiniwa walivyojibu maswali ya mtihani.

Taarifa hii ni tathmini ambayo pamoja na mambo mengine, inaonesha mafanikio katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Stadi za Kazi. Kimsingi, majibu ya watahiniwa katika maswali ya mtihani ni uthibitisho wa kipi mfumo wa elimu uliweza au ulishindwa kuwapa wanafunzi wawapo katika mafunzo ya Ualimu katika daraja hili.

Uchambuzi uliowasilishwa katika taarifa hii una lengo la kuchangia katika kuelewa sababu za watahiniwa kufanya vizuri au vibaya katika kujibu maswali ya mtihani. Sababu zilizowafanya watahiniwa wachache kushindwa kupata alama za juu katika baadhi ya maswali ni pamoja na kushindwa kuelewa matakwa ya maswali, kukosa maarifa ya kutosha kuhusu dhana zilizopimwa, kutoa maelezo yasiyotosheleza na uelewa mdogo katika kujibu maswali ya insha. Baraza linaamini kuwa mrejesho huu utawawezesha viongozi wa elimu, wamiliki wa vyuo, viongozi wa vyuo, wathibiti ubora wa elimu, wakufunzi na wanachuo kupata mbinu muafaka katika kuboresha ufaulu wa watahiniwa katika mitihani ijayo inayoendeshwa na Baraza la Mitihani la Tanzania. Mwisho, Baraza la Mitihani la Tanzania linapenda kuwashukuru wale wote walioshiriki katika kuandaa taarifa hii.

Dkt. Charles E. Msonde
**KATIBU MTENDAJI**

# 1.0 UTANGULIZI

Taarifa hii ya uchambuzi inawasilisha ufaulu wa watahiniwa wa mtihani wa Ualimu Daraja la A (GATCE) somo la 634 Stadi za Kazi uliofanyika Mei 2019. Mtihani huu ulizingatia muhtasari wa somo la Stadi za Kazi wa mwaka 2009.

Mtihani huu ulikuwa na jumla ya maswali 16 yaliyogawanywa katika sehemu A, B na C. Sehemu A ilikuwa na maswali 10 ya majibu mafupi kutoka katika mada za taaluma na ufundishaji na mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote. Sehemu B ilikuwa na maswali 3 ya insha kutoka katika mada za taaluma ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali 2. Aidha, sehemu C ilikuwa na maswali 3 ya insha kutoka katika mada za ufundishaji na mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali 2. Sehemu A ilikuwa na jumla ya alama 40 wakati sehemu B na C zilikuwa na jumla ya alama 30 kila moja.

Uchambuzi wa matokeo unaonesha kuwa watahiniwa 4,202 (99.17%) walifanya mtihani huu ambapo miongoni mwao, watahiniwa 4,198 (99.98%) walifaulu kwa kupata gredi A hadi D wakati mtahiniwa 1 (0.02%) alifeli kwa kupata gredi F. Hata hivyo, matokeo ya watahiniwa 3 yalizuiliwa kutokana na sababu mbalimbali. Kiwango cha kufaulu kwa mwaka 2019 kimepanda kwa asilimia 0.06 ukilinganisha na mwaka 2018 ambapo kati ya watahiniwa 4,843 waliofanya mtihani huo, watahiniwa 4,819 (99.92%) walifaulu na watahiniwa 4 (0.08%) walifeli.

Katika taarifa hii, viwango vya kufaulu kwa watahiniwa vimegawanywa katika makundi matatu ambayo ni “vizuri", "wastani" na "hafifu". Ufaulu wa kiwango kizuri ni kuanzia asilimia 70 hadi 100, kiwango cha wastani ni kuanzia asilimia 40 hadi 69 na ufaulu wa kiwango hafifu ni kuanzia asilimia 0 hadi 39. Aidha, chati na majedwali ya viwango vya kufaulu yameambatishwa ili kuonesha ufaulu wa watahiniwa ambapo rangi ya kijani inawakilisha ufaulu wa kiwango kizuri, rangi ya njano inawakilisha ufaulu wa kiwango cha wastani na ufaulu wa kiwango hafifu unawakilishwa na rangi nyekundu.

Taarifa hii inatoa uchambuzi wa kila swali ikionesha kile kilichotakiwa kufanywa na watahiniwa, jinsi watahiniwa walivyojibu swali, ufaulu wa kila swali na sababu zilizowafanya watahiniwa kupata ufaulu mzuri, wastani au hafifu katika majibu yao. Sampuli za majibu ya watahiniwa zimeambatanishwa ili kuonesha kile walichofanya.

## 2.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA SWALI

### 2.1 SEHEMU A

Sehemu A ilikuwa na maswali 10 (swali la 1 hadi 10) ya lazima kutoka katika mada mbalimbali. Kila swali katika sehemu hii lilikuwa na jumla ya alama 4. Viwango vya kufaulu kwa maswali ya sehemu hii ilikuwa kama ifuatavyo: Ufaulu mzuri ulianzia alama 3 hadi 4, ufaulu wa wastani ulianzia alama 2 hadi 2.5 na ufaulu hafifu ulianzia alama 0 hadi 1.5.

#### 2.1.1 Swali la 1: Usanii wa picha, chapa, maumbo na mapambo


Katika swali hili mtahiniwa alitakiwa kueleza kwa kifupi mambo manne ya kuzingatia katika upambaji wa nguo kwa kutumia rangi. Watahiniwa wote (100%) walifanya swali hili. Miongoni mwao watahiniwa 4,190 (99.7%) walipata kuanzia alama 0 hadi 1, tisa (0.2%) walipata kuanzia alama 2 na watatu (0.1%) walipata kuanzia alama 4. Kiwango cha kufaulu katika swali hili kilikuwa hafifu kwani watahiniwa 12 (99.7%) ndio walipata kuanzia alama 2 hadi 4. Jedwali Na. 1 linaonesha kiwango cha kufaulu katika swali hili.

| Alama | Asilimia ya Watahiniwa |
|---|---|
| 0 – 1.5 | 99.7 |
| 2 – 2.5 | 0.2 |
| 3 - 4 | 0.1 |

**Jedwali Na. 1:** *Kufaulu kwa watahiniwa katika swali la 1.*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa umeonesha kuwa watahiniwa 3,966 (94.4%) walipata alama 0 kutokana na sababu mbalimbali. Baadhi yao walionesha kushindwa kuelewa matakwa ya swali. Waliandika hatua za kufuata wakati wa kupamba kitambaa, nguo au kifaa cha ususi kwa kutumia rangi badala ya mambo ya kuzingatia katika upambaji wa nguo kwa kutumia rangi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika hoja zifuatazo: *andaa vifaa vya kuwezesha kupamba kama rangi, nguo, meza, maji, brashi, beseni n.k, changanya rangi kulingana na jinsi unavyotaka kupendezesha nguo yako mfano, msingi, upili au msigishano, andaa sehemu inayotumika kufanyia shughuli hiyo, mfano nafasi katika chumba* na *paka rangi nguo ulizoandaa mpaka zilete mvuto unaotaka.* Watahiniwa wengine waliandika vifaa vinavyotumika kupamba nguo kwa kutumia

rangi badala ya mambo ya kuzingatia katika upambaji wa nguo kwa kutumia rangi. Walitaja vifaa kama: *kamba za kuanikia, rangi, beseni, nguo, brashi* na *maji*. Kundi lingine la watahiniwa walikosa maarifa ya kutosha katika dhana ya upambaji wa nguo, hivyo waliandika hoja ambazo sio sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika: *kuhakikisha mapambo yanaendana na nguo, kutumia rangi za aina tofautitofauti ili kuleta mvuto, kuhakikisha rangi ya nguo haipauki* na *kupamba kwa kuelekea upande mmoja*. Mtahiniwa mwingine aliandika majibu yafuatayo ambayo sio sahihi: *nguo ni lazima iwe yenye rangi tofauti tofauti, nguo iwe safi, nguo iwe yenye mvuto* na *nguo isiwe yenye kung'aa sana*. Watahiniwa waliopata alama 1 ambao ni asilimia 5.3 waliweza kuelezea hoja moja kwa usahihi. Kielelezo Na. 1.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyepata alama za chini katika swali hili.


1. (i) Rangi: katika upambaji wa nguo kwa kutumia rangi ni vema uzingatie upatikanaji wa rangi hizo.
(ii) Nguo au vitambaa: katika kupamba nguo kwa kutumia rangi ni vema uzingatie uwepo wa nguo utakazozipamba.
(iii) Vifaa vya rangi: Ni vema kuwepo na vifaa vitakavyotumika kuwekea rangi mfano beseni na ndoo.
(iv) Kamba au waya: Hii ni kwa ajili ya kuanikia nguo baada ya kupamba.

**Kielelezo Na. 1.1:** *Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 1.*

Katika Kielelezo Na. 1.1, mtahiniwa alijibu swali hili kwa kueleza vifaa vinavohitajika wakati wa kupamba nguo kwa kutumia rangi badala ya mambo ya kuzingatia katika upambaji wa nguo kwa kutumia rangi. Hii ilisababishwa na mtahiniwa huyu kushindwa kuelewa matakwa ya swali.

Watahiniwa wachache (0.3%) walipata alama za wastani na nzuri katika swali hili. Watahiniwa hao waliweza kubaini kuwa wakati wa kupamba nguo kwa kutumia rangi inapaswa: *kuzingatia na kufuata maelekezo ya matumizi ya rangi yaliyoko juu ya kifungashio cha rangi, kuchagua rangi/makunzi sahihi ya rangi, muda wa kuweka kitambaa kwenye maji hadi kukauka, umakini katika kazi nzima ya kupamba nguo kwa kutumia*

*rangi ili kuepuka kuharibu kitambaa na rangi* na *pia kuzingatia usafi na usalama wakati wa upambaji wa nguo ili kuepuka kuumia na kuchafuka*. Watahiniwa hao walionesha kuwa na maarifa ya kutosha katika mada husika na waliweza kuelewa matakwa ya swali. Aidha, baadhi ya watahiniwa katika kundi hili walishindwa kupata alama zote 4 kwa sababu walitoa maelezo ambayo hayakujitosheleza katika baadhi ya hoja. Wengine waliandika hoja sahihi na ambazo sio sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa pamoja na kutaja hoja sahihi mbili, aliandika pia hoja mbili zisizokuwa sahihi ambazo ni: *angalia sehemu za kupaka rangi ili ivutie* na *kuweka rangi vizuri ili isitiririke* jambo lililopelekea kushindwa kupata alama zote.

### 2.1.2 Swali la 2: Upimaji


Swali lilimtaka mtahiniwa kuonesha umuhimu wa upimaji katika somo la Stadi za Kazi kwa kutumia hoja nne. Kati ya watahiniwa 4,201 (100%) waliofanya swali hili, 4,178 (99.5%) walipata kuanzia alama 3 hadi 4, 5 (0.1%) walipata kuanzia alama 2 hadi 2.5 na 18 (0.4%) walipata kuanzia alama 0 hadi 1.5. Kwa ujumla, swali hili lilifanyika vizuri kutokana na idadi kubwa ya watahiniwa ambao ni 4,183 (99.6%) kupata alama 2 na zaidi kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 2.

| Alama | Asilimia ya Watahiniwa |
|---|---|
| 0 – 1.5 | 0.4 |
| 2 – 2.5 | 0.1 |
| 3 - 4 | 99.5 |

**Jedwali Na. 2:** *Kufaulu kwa watahiniwa katika swali la 2.*

Watahiniwa waliopata ufaulu mzuri waliweza kuonesha kwa usahihi umuhimu wa upimaji katika somo la Stadi za Kazi kwa kuandika hoja nne. Hoja zilizoandikwa na watahiniwa hao ni pamoja na hizi zifuatazo: *kutafuta ufumbuzi wa matatizo yanayowakabili wanafunzi wakati wa kujifunza, mwalimu kuweza kubadilisha mbinu za kufundishia na zana za kufundishia na kujifunzia, kutambua matatizo yanayowapata wanafunzi wakati wa kujifunza somo, wazazi na walezi kuweza kutambua maendeleo ya watoto wao kitaaluma, hutumika kupandisha darasa kwa wanafunzi kutoka darasa la chini kwenda la juu, kugundua malengo ya somo ambayo yanapaswa kurekebishwa ili wanafunzi waweze kuyafanikisha* na *kubaini wanafunzi wenye matatizo ya kuelewa somo.* Ufaulu mzuri katika swali hili ulitokana na watahiniwa kuwa na uelewa mzuri katika dhana iliyopimwa na


kuelewa matakwa ya swali. Waliweza pia kuhusianisha maarifa ya darasani na mazoezi kwa vitendo ambapo walishuhudia umuhimu wa kuwapima wanafunzi katika somo la Stadi za Kazi. Hata hivyo, watahiniwa waliopata alama 3 waliandika hoja tatu sahihi badala ya nne. Kielelezo Na. 2.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kujibu swali hili kwa usahihi.


2. i) Kutambua maendeleo ya wanafunzi baada ya kupima - Mwalimu anaweza kubaini maendeleo au mapungufu ya wanafunzi wake ili kuwasaidia.
ii) Kumsaidia mwalimu kubaini wanafunzi wenye matatizo katika kujifunza yaani mahitaji maalumu.
iii) Unasaidia katika kupanda darasa / daraja katika ngazi ya elimu, kutokana na kufanya vizuri mwanafunzi anaweza kupanda daraja.
iv) Kumsaidia mwalimu kufanya tathmini ya somo lake, baada ya upimaji mwalimu anaweza kufahamu ni kwa kiwango gani somo lake limefanikiwa au kutofanikiwa.

**Kielelezo Na. 2.1:** *Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 2.*

Katika Kielelezo Na. 2.1, mtahiniwa aliweza kufafanua kwa usahihi umuhimu wa upimaji katika somo la Stadi za Kazi.

Pamoja na watahiniwa kufanya vizuri swali hili, watahiniwa 18 (0.4%) walishindwa kujibu swali hili kwa ufasaha kutokana na kukosa maarifa kuhusu mada ya Upimaji na kushindwa kuhawilisha maarifa kutoka katika masomo mengine ambako mada hii pia hufundishwa. Uchambuzi ulionesha kuwa watahiniwa waliandika majibu yaliyokuwa kinyume na umuhimu wa upimaji katika somo la Stadi za Kazi, kama vile: *kuwagawa wanafunzi katika makundi, humwezesha mwanafunzi kuongeza bidii katika masomo, huwasaidia walimu kufanya ulinganyifu wa wanafunzi, husaidia kuonyesha madaraja ya ufaulu, husaidia kujaza taarifa katika fomu ya maendeleo ya mwanafunzi* na *upimaji husaidia kupata viongozi bora*. Kielelezo Na. 2.2 ni sampuli ya jibu kutoka kwenye skripti ya mtahiniwa aliyejibu vibaya swali.



2. (i) Kumwezesha mwalimu kupima uwezo wa wanafunzi.
(ii) Upimaji unamwezesha mwanafunzi kuongeza bidii.
(iii) Upimaji unamsaidia mwalimu kujua matatizo mbalimbali ya wanafunzi.
(iv) Upimaji unasaidia kupanga viwango vya ufaulu.

**Kielelezo Na. 2.2:** *Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 2.*

Katika Kielelezo Na. 2.2, mtahiniwa alishindwa kuonesha kwa usahihi umuhimu wa upimaji katika somo la Stadi za Kazi.

### 2.1.3 Swali la 3: Ususi


Katika swali hili mtahiniwa alitakiwa kubainisha faida nne za kutumia vifaa vya asili katika ususi. Jumla ya watahiniwa 4,202 (100%) walifanya swali hili na kati yao 3,947 (93.9%) walipata kuanzia alama 3 hadi 4, watahiniwa 143 (3.4%) walipata kuanzia alama 2 hadi 2.5 na wengine 114 (2.7%) walipata kuanzia alama 0 hadi 1.5. Takwimu hizi zinaonesha kuwa kiwango cha kufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri kwa sababu watahiniwa 4,090 (97.3%) walipata alama kuanzia 2 hadi 4 kama inavyoonekana kwenye Chati Na. 1.




**Chati Na. 1:** *Kufaulu kwa watahiniwa katika swali la 3.*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa umeonesha kuwa watahiniwa wengi waliopata ufaulu mzuri walionekana kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu

dhana ya vifaa vinavyotumika katika ususi. Waliweza kueleza kwa usahihi faida za kutumia vifaa vya asili katika ususi kama vile: *kupatikana kwa gharama ndogo na wakati mwingine bila gharama, kupatikana kwa urahisi katika mazingira tunamoishi, kutumika kutengeneza vifani vinavyotangaza utamaduni wetu, kusaidia upatikanaji wa vifani kwa haraka pale vinapohitajika* na *ni rahisi kuvitumia kutengeneza vifani mbalimbali.* Kielelezo Na. 3.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.


3. i/ Ina saidia kuepusha gharama
ii/ Ina saidia kutangaza utamaduni wa jamii fulani
iii/ Ina rahisisha upatikanaji wa vifani kwa haraka
iv/ Ina saidia kukuza ubunifu wa kutumia vifaa
vya asili


**Kielelezo Na. 3.1:** *Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 3.*

Katika Kielelezo Na. 3.1, mtahiniwa aliweza kubainisha kwa usahihi faida za kutumia vifaa vya asili katika ususi.

Aidha, watahiniwa waliopata ufaulu wa wastani walitoa majibu ambayo hayakukidhi mahitaji ya swali. Baadhi yao waliandika hoja sahihi na zisizo sahihi. Kwa mfano, pamoja na hoja mbili kuandikwa kwa usahihi, baadhi ya watahiniwa waliandika hoja zisizo sahihi, kama vile: *kufanywa kwa ubunifu, kuleta mvuto zaidi, kusafisha mazingira*, *kukosa fedha za kununulia vifaa vya kisasa* na *kukosa ujuzi wa kutumia vifaa vya kisasa*. Majibu haya yalisababisha wanafunzt kushindwa kupata alama za juu. Watahiniwa wengine waliandika baadhi ya hoja mara mbili. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika, *hutengeneza vifaa imara* na *vifaa vya asili hutengeneza vifaa vinavyodumu kwa muda mrefu* kama hoja mbili tofauti wakati kimsingi ni hoja moja.

Kwa upande mwingine, pamoja na ufaulu mzuri wa watahiniwa katika swali hili, watahiniwa wachache (2.4%) walipata ufaulu hafifu. Uchambuzi umeonesha kuwa baadhi ya watahiniwa hao walishindwa kuelewa matakwa ya swali. Kwa mfano, baadhi ya watahiniwa walifasili swali vibaya kwani badala ya kubainisha faida za kutumia vifaa vya asili katika ususi, walitaja aina za vifaa vya asili vinavyotumika katika ususi, kama vile: *kindu, kili,*

*katani, majani ya migomba, matawi* na *majani ya minyaa*. Watahiniwa wengine walibainisha matumizi ya vifani vinavyotokana na vifaa vya asili vya ususi kwa kuandika: *hutumika kuanikia mazao mfano mikeka, kujikinga jua kwa kuvaa kofia, kufunika chakula kwa kawa* na *kubebea mizigo mfano kutumia vikapu*. Baadhi ya watahiniwa walikosa maarifa kuhusu mada hii, hivyo waliandika majibu yasiyo sahihi, kama vile: *kupata ajira, kujenga kumbukumbu, kuongeza kipato, kukuza sanaa ya ususi, kupata ujuzi* na *kufanya matumizi sahihi ya vifaa*. Watahiniwa hawa walishindwa kuelewa kuwa hata kutumia vifaa ambavyo sio vya asili katika ususi husaidia *kupata ajira, kuongeza kipato* na *kupata ujuzi*. Kielelezo Na. 3.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyepata ufaulu hafifu katika swali hili.



03 a. Ukili
b. Matawi
c. Katani
d. Majani

**Kielelezo Na. 3.2:** *Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 3.*

Katika Kielelezo Na. 3.2, mtahiniwa alitaja vifaa vya asili vinavyotumika katika ususi badala ya faida za kutumia vifaa vya asili na hivyo kupata alama za chini.


### 2.1.4 Swali la 4: Maandalizi ya ufundishaji

Swali lilimtaka mtahiniwa kutaja mambo manne ya kuzingatia katika kufaragua zana za kufundishia na kujifunzia somo la Stadi za Kazi. Watahiniwa wote (100%) walifanya swali hili. Kati yao, watahiniwa 4,148 (98.7%) walipata kuanzia alama 0 hadi 1.5, watahiniwa 36 (0.9%) walipata kuanzia alama 2 hadi 2.5, na wengine 18 (0.4%) walipata kuanzia alama 3 hadi 4. Kwa ujumla, ufaulu katika swali hili ulikuwa hafifu kwa kuwa idadi ya watahiniwa walioweza kupata kuanzia alama 2 hadi 4 ni 54 (1.3%) tu. Kiwango cha kufaulu katika swali hili ni kama inavyoonekana kwenye Chati Na. 2.




**Chati Na. 2:** *Kufaulu kwa watahiniwa katika swali la 4.*

Watahiniwa waliopata ufaulu hafifu walionesha kuandika majibu tofauti na swali lilivyotaka. Wengi wao walitaja vigezo mbalimbali vya kuzingatia wakati wa kutengeneza zana za kufundishia na kujifunzia, kama vile: *idadi ya walengwa/wanafunzi, uwezo wa wanafunzi, zana ziendane na maudhui ya somo, umri wa wanafunzi, zingatia uelewa wa wanafunzi na ukubwa wa darasa, ziendane na lengo mahususi, ziwe zinabebeka na kuhifadhika kirahisi, ziwe imara* na *zingatia ujuzi wa mwalimu*. Watahiniwa wachache walionesha kukosa maarifa ya kutosha katika mada husika, hivyo kushindwa kuandika majibu sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika: *kushirikisha wanafunzi kutengeneza, matumizi ya zana kubwa, zingatia vipimo na mshono* na *tunza zana sehemu safi na salama*. Kielelezo Na. 4.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyewasilisha jibu lisilohusiana na matakwa ya swali.



| | | |
|---|---|---|
| 04 | (i) Malengo Mahususi | |
| | (ii) Umri wa wanafunzi | |
| | (iii) Idadi ya wanafunzi | |
| | (iv) Uelewa wa wanafunzi | |
| | | |

**Kielelezo Na. 4.1:** *Sampuli ya jibu lisilo katika swali ls 4.*


Katika Kielelezo Na. 4.1, mtahiniwa alitaja vigezo vya kuzingatia wakati wa kutengeneza zana badala ya vigezo vya kuzingatia wakati wa kufaragua zana za kufundishia na kujifunzia somo la Stadi za Kazi.

Aidha, watahiniwa waliokuwa na ufaulu wa wastani katika swali hili walitoa majibu ambayo hayakujitosheleza, hivyo kushindwa kupata alama zote. Baadhi yao walichanganya hoja sahihi na ambazo sio sahihi. katika kujibu swali hili. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliorodhesha hoja sahihi mbili na mbili zisizo sahihi kwa kuandika: *mwalimu kuzingatia uwezo wa wanafunzi katika kubuni mambo* na *kuzingatia ukubwa wa chumba cha kufundishia*. Watahiniwa wengine walitaja hoja mbili badala ya nne kama swali lilivyotaka kutokana na kukosa maarifa ya kutosha kuhusu mada ya maandalizi ya ufundishaji au kushindwa kuelewa matakwa ya swali.

Kwa upande mwingine, watahiniwa wachache waliopata ufaulu mzuri walidhihirisha kuwa na maarifa ya kutosha katika dhana ya kufaragua zana za kufundishia na kujifunzia somo la Stadi za Kazi. Waliweza kueleza kuwa wakati wa kufaragua zana za kufundishia na kujifunzia somo hili, ni lazima kuzingatia mambo yafuatayo: *kutumia makunzi yanayodumu kwa muda mrefu, matumizi ya vitu visivyokuwa yakinifu, kitu kilichofaraguliwa lazima kilandane na kitu halisi* na *kutumia njia rahisi ya ufaraguaji wa zana*. Aidha, watahiniwa walioshindwa kupata alama zote 4 waliandika kwa usahihi hoja tatu kati ya nne.


### 2.1.5 Swali la 5: Muziki

Katika swali hili mtahiniwa alitakiwa kuorodhesha tahadhari nne za kuchukua wakati wa mazoezi ya kuimba. Uchambuzi wa takwimu za matokeo umeonesha kuwa watahiniwa wote (100%) walifanya swali hili. Kati yao, watahiniwa 3,584 (85.3%) walipata kuanzia alama 0 hadi 1.5, watahiniwa 267 (6.3%) walipata kuanzia alama 2 hadi 2.5 na wengine 351 (8.4%) walipata kuanzia alama 3 hadi 4. Takwimu zinaonesha kiwango hafifu cha kufaulu katika swali hili kwani ni watahiniwa 618 (14.7%) tu ndio waliweza kupata alama 2 na zaidi. Chati Na. 3 inawasilisha kiwango cha kufaulu katika swali hili.




**Chati Na. 3:** *Kufaulu kwa watahiniwa katika swali la 5.*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa umeonesha kuwa watahiniwa wengi waliopata alama 0 hadi 1.5 walionesha kuwa na uelewa mdogo katika dhana ya uimbaji, hivyo walikuwa wakizitaja hoja kwa kubahatisha. Kwa mfano, mtahiniwa aliandika hoja zifuatazo ambazo hazikuwa na uhusiano na matakwa ya swali: *kuepuka mwingiliano wa mambo mengi kichwani, kuepuka kupoteza maudhui ya wimbo, kuwa na chumba chenye vioo ambavyo havipitishi sauti* na *kuepuka kupoteza umakini*. Mtahiniwa mwingine aliandika hoja zifuatazo: *kuzingatia jinsia, nyimbo ziendane na wakati uliopo, waimbaji wapangwe kulingana na sauti* na *kuimba wakati wamesimama wima*. Ilibainika pia kuwa watahiniwa wachache katika kundi hili walishindwa kuelewa matakwa ya swali ambapo walijibu tofauti kabisa na walivyoulizwa. Kwa mfano, mtahiniwa alielewa tahadhari za kuchukua wakati wa mazoezi ya kuimba kama tahadhari za kuchukua wakati wa mazoezi ya kukimbia, hivyo aliandika hoja zifuatazo: *kuvaa nguo za michezo (zisizobana), kuvaa viatu vya kukimbilia (raba), kukimbia ukiwa umekunja ngumi/vidole vya mikono* na *kukimbia ukiwa umefumba mdomo*. Kielelezo Na. 5.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vibaya swali hili.




5 i Kuepuka kuwa na mwingiliano wa mambo mengi kichwani
ii Kuepuka kupoteza maudhui ya wimbo
iii kuwa na chumba chenye vioo ambavyo havipitishi sauti kutoka kwenda nje
iv Kuepuka kupoteza umakini

**Kielelezo Na. 5.1:** *Sampuli hoja zisizokuwa sahihi katika swali la 5.*

Katika Kielelezo Na. 5.1, mtahiniwa aliandika hoja zisizohusiana na tahadhari za kuchukua wakati wa mazoezi ya kuimba.

Watahiniwa waliopata alama za wastani katika swali hili ambao ni asilimia 6.3 waliweza kuandika hoja mbili tu ambazo ni sahihi badala ya nne. Wengine walishindwa kutoa maelezo ya kutosheleza katika baadhi ya hoja walizotaja. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika hoja zifuatazo: *usile vyakula vya baridi, kunywa maji mengi* na *kuwa na muda wa kupumzika.* Hata hivyo, alishindwa kubainisha muda sahihi wa kuyafanya mambo aliyoyataja ambao ni kabla ya kuanza mazoezi ya kuimba.

Uchambuzi zaidi umeonesha kuwa watahiniwa wachache (8.4%) waliopata alama za juu, walitumia ujuzi na maarifa waliyokuwa nayo kueleza tahadhari za kuchukua wakati wa mazoezi ya kuimba ambazo ni pamoja na hizi zifuatazo: *kunywa maji ya kutosha kabla ya mazoezi na wawe nayo wakati wa mazoezi, wasiimbe kwa sauti ya juu sana, kuanzia kufanyia mazoezi wimbo ulio rahisi, kula mlo laini saa chache kabla ya kuanza mazoezi, kupumzika vya kutosha kabla ya kuanza kufanya mazoezi ya kuimba* na *kutokula vyakula vya sukari na baridi kabla ya kuanza mazoezi ya kuimba*. Kielelezo Na. 5.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.



5 i) Kuwa na Maji ya kulainisha koo wakati wa uimbaji pale linapokauka
ii) Kutoshiba sana Maana ukishiba sauti huwa hazitoki vizuri
iii) kutokula vyakula vya baridi kabla ya mazoezi
iv) kutoimba kwa sauti ya juu sana.

**Kielelezo Na. 5.2:** *Sampuli ya jibu sahihi katika swali ka 5.*

Katika Kielelezo Na. 5.2, mtahiniwa aliweza kuorodhesha tahadhari za kuchukua wakati wa mazoezi ya kuimba.


### 2.1.6 Swali la 6: Ufundishaji

Swali lilimtaka mtahiniwa kueleza upungufu wa kutumia njia ya mhadhara kufundishia mada ya "Ushoni wa nguo". Swali hili lilifanywa na watahiniwa wote (100%). Miongoni mwao, watahiniwa 3,451 (82.1%) walipata kuanzia alama 3 hadi 4 na wengine 483 (11.5%) walipata kuanzia alama 2 hadi 2.5. Aidha, watahiniwa 268 (6.4%) walipata kuanzia alama 0 hadi 2.5. Kiwango cha kufaulu kilikuwa ni kizuri kama inavyoonekana kwenye Chati Na. 4.




**Chati Na. 4:** *Kufaulu kwa watahiniwa katika swali la 6.*

Watahiniwa waliopata alama 3 hadi 4 walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mbinu bora za kufundishia mada ya Ushoni wa nguo. Hii iliwawezesha kueleza kwa ufasaha kuwa kwa kutumia njia ya mhadhara: *somo halitawavutia wanafunzi kwani njia hii haiwashirikishi katika kujifunza, njia hii haitakuza ujuzi wa kuuliza, kufanya hitimisho la busara na kudadisi mambo yanayohusiana na mada hii, wanafunzi hawataweza kufanya mazoezi ya kushona na kuona matumizi ya vifaa mbalimbali vya ushoni* na pia, *kwa wanafunzi wasio na ujuzi wa kuchukua nukuu na kusikiliza itakuwa vigumu kwao hata kuandika nukuu za somo hili*. Kielelezo Na. 6.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.


06 i) Somo kutoeleweka vinzuri; kutokana na mwalimu-
ndiye anayekuwa mhusika mkuu wa kuelezea somo
kuanzia mwanzo hadi mwisho

ii) Mwanafunzi kutojifunza kwa vitendo; Hata kama
mwalimu atakuwa na zana ataishia kuitumia pek
e yake bila kumshirikisha mwanafunzi

iii) Haitakuza ujuzi wa mwanafunzi: Kwa sabab
bu atakuwa hajashiriki katika kujaribu namn
a ya kushona nguo kwa kutumia mkono.

iv) Haitarahisisha ufundishaji na ujifunzaji; Hii hutok
ana na kwa vile mwalimu atakavyokuwa akijis
hirikisha peke yake hivyo kuchukua muda m
wingi kufundisha mada hiyo.


**Kielelezo Na. 6.1:** *Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 6.*

Katika Kielelezo Na. 6.1, mtahiniwa aliweza kueleza kwa kifupi madhara ya kutumia njia ya mhadhara kufundishia mada ya "Ushoni wa nguo".

Watahiniwa wengi waliopata ufaulu wa wastani waliweza kuandika hoja 2 kwa usahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja pamoja na kutaja hoja sahihi mbili, alitaja pia hoja mbili zisizokuwa sahihi ambapo aliandika: *inatumia gharama kubwa* na *inahitaji muda mrefu kufundisha*. Mtahiniwa huyu alishindwa kuelewa kuwa hizi ni hasara za kutumia njia ya ziara kufundishia na sio upungufu wa kutumia njia ya mhadhara kufundishia mada ya Ushoni wa nguo. Watahiniwa wengine waliandika hoja moja mara mbili. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika: *njia hii huwafanya wanafunzi kutovutiwa na somo hili* na *wanafunzi hawashirikishwi katika ujifunzaji kwani mwalimu ndiye msemaji wa kila kitu* ambazo kimsingi ni hoja moja kwa sababu wanafunzi kutovutiwa na somo inatokana na kutoshirikishwa katika ujifunzaji.

Watahiniwa wachache waliopata ufaulu hafifu walionesha kukosa maarifa ya kutosha kuhusu mada hii. Hali hii ilisababisha wengi wao kuandika hoja ambazo hazikuhusiana na swali, kama vile: *walimu wengi hushindwa*

*kufundisha mada hii, upungufu wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia, idadi kubwa ya wanafunzi katika kifaa kimoja kwa sababu vifaa huuzwa bei kubwa, njia hii hupoteza muda mrefu kutokana na idadi kubwa ya wanafunzi, wanafunzi kuwa wengi na hivyo kuweza kutoroka kipindi bila kuonekana* na *mwalimu kushindwa kulimudu darasa*. Kielelezo Na. 6.2 kinaonesha sampuli ya jibu ya mtahiniwa aliyepata ufaulu hafifu katika swali hili.


6. (i) Upungufu wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia. kutokana na idadi kubwa ya wanafunzi.
(ii) Idadi kubwa katika kifaa kimoja cha kujifunzia kutokana na vifaa vyenyewe kuwa vichache.
(iii) Kushindwa kulimudu darasa. pia mwalimu atashindwa kulimudu darasa kutokana na idadi kubwa ya wanafunzi.
(iv) Hupoteza muda mwingi. kutokana na idadi kuwa kubwa hivyo mwaalimu atatumia muda mwingi.

**Kielelezo Na. 6.2:** *Sampuli ya jibu ambalo sio sahihi katika swali la 6.*

Katika Kielelezo Na. 6.2, mtahiniwa alieleza hoja ambazo hazina uhusiano na swali hili kutokana na kukosa maarifa ya kutosha kuhusu mada ya "Ushoni nguo".


### 2.1.7 Swali la 7: Upishi

Swali lilimtaka mtahiniwa kutaja madhara manne yanayoweza kutokea endapo kanuni za usafi na usalama wa chumba cha kupikia hazitazingatiwa. Jumla ya watahiniwa 4,200 (100%) walifanya swali hili. Kati yao, watahiniwa 4,080 (97.1%) walipata kuanzia alama 3 hadi 4, watahiniwa 83 (2%) walipata kuanzia alama 2 hadi 2.5 na wengine 37 (0.9%) walipata kuanzia alama 0 hadi 1.5. Watahiniwa waliofaulu kwa kupata alama kuanzia 2 hadi 4 ni 4,163 (99.1%), hivyo kufanya kiwango cha kufaulu katika swali hili kuwa ni kizuri. Jedwali Na. 3 linaonesha kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swai hili.

| Alama | Asilimia ya Watahiniwa |
|---|---|
| 0 – 1.5 | 0.9 |
| 2 – 2.5 | 2.0 |
| 3 - 4 | 97.1 |

**Jedwali Na. 3:** *Kufaulu kwa watahiniwa katika swali la 7.*

Watahiniwa wengi (97.1%) walionesha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya kanuni za usafi na usalama wa chumba cha kupikia. Walielewa kuwa endapo kanuni za usafi na usalama wa chumba cha kupikia hazitazingatiwa, madhara yafuatayo yanaweza kutokea: *mpishi kuumia kwa kuanguka kutokana na kuteleza au kujikwaa katika sakafu yenye mashimo, kupata magonjwa kutokana na vyombo na mazingira ya chumba cha kupikia kuwa na uchafu, vyombo kuvunjika kama havitapangwa/kuwekwa vizuri, chakula kuharibika mapema kutokana na uchafu, kutokea ajali za moto zinazoweza kuunguza jengo, mali na vifaa vingine* na *kuwepo kwa mazalia na maficho ya wadudu mfano mende na nzi*. Watahiniwa waliopata kuanzia alama 3 hadi 4 waliweza kuandika hoja tatu kwa usahihi. Kielelezo Na. 7.1 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili vizuri.


7. (i) Magonjwa mfano Kipindupindu.
(ii) Chakula Kuharibika haraka.
(iii) Ajali kutokana na mpangilio mbaya wa vitu.
(iv) Wadudu mfano inzi Kuzaliana katika jiko.


**Kielelezo Na. 7.1:** *Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 7.*

Katika Kielelezo Na. 7.1, mtahiniwa aliyeweza kutaja madhara yanayoweza kutokea endapo kanuni za usafi na usalama wa chumba cha kupikia hazitazingatiwa.

Watahiniwa waliopata ufaulu wa wastani walichukulia hoja moja kama hoja mbili au tatu tofauti. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika: *kufanya sehemu ya wadudu kuzaliana* na *wadudu mfano mende huweza kujificha* kama hoja mbili tofauti wakati kimsingi ni hoja moja ya *kuwa na mazalia na maficho ya wadudu kama mende*. Mtahiniwa mwingine aliandika: *husababisa magonjwa*, *husababisha homa ya matumbo* na *husababisha kipindu pindu*. Mtahiniwa huyu alishindwa kuelewa kuwa

homa ya matumbo na kipindupindu ni mifano ya magonjwa yanayoweza kutokea endapo kanuni za usafi na usalama katika chumba cha kupikia hazitazingatiwa. Watahiniwa wengine walitaja madhara sahihi lakini hawakutoa maelezo yoyote. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika: *ajali, uchafu, magonjwa na uharibifu* lakini hakutoa maelezo yoyote.

Watahiniwa wachache (0.9%) waliopata kuanzia alama 0 hadi 1.5, walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada husika. Waliandika hoja ambazo sio sahihi, kama vile: *chakula kuwa na mchanga, kufungiwa biashara, kukosa wateja, kupata homa, wateja kukosa imani na chakula chako, kutozwa faini* na *kufunga biashara*. Baadhi ya watahiniwa katika kundi hili waliweza kutaja hoja moja kwa usahihi, hivyo kupata alama 1 kati ya 4. Kielelezo Na. 7.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyepata alama za chini katika swali hili.


7 (i) Kupata ugonjwa wa homa
(ii) chakula kuwa na mchanga
(iii) Kulipishwa Faini na bi: afya/bwana afya
(iv) Kupotea kwa walaji wa chakula
(v) Kupata majeraha


**Kielelezo Na. 7.2:** *Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 7.*

Katika Kielelezo Na. 7.2, mtahiniwa alishindwa kutaja madhara sahihi yanayoweza kutokea endapo kanuni za usafi na usalama wa chumba cha kupikia hazitazingatiwa. Hata hivyo, mtahiniwa huyu aliandika hoja tano badala ya nne zilizotakiwa kwenye swali.

### 2.1.8 Swali la 8: Ufundishaji


Katika swali hili, mtahiniwa alitakiwa kueleza kwa kifupi mbinu nne zinazoweza kutumika kufundishia na kujifunzia dhana ya "Uimbaji wa solfa". Jumla ya watahiniwa 4,202 (100%) walifanya swali hili. Watahiniwa 2,494 (59.4%) walipata kuanzia alama 3 hadi 4, watahiniwa 1,041 (24.7%) walipata kuanzia alama 2 hadi 2.5 na wengine 667 (15.9%) walipata kuanzia alama 0 hadi 1.5. Kwa ujumla, kiwango cha kufaulu kilikuwa ni kizuri kwa sababu watahiniwa 3,535 (84.1%) walipata kuanzia

alama 2 hadi 4. Chati Na. 5 inaonesha kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili.





**Chati Na. 5:** *Kufaulu kwa watahiniwa katika swali la 8.*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa ulibaini kuwa watahiniwa waliopata alama 3 hadi 4 walikuwa na maarifa na ujuzi wa kutosha katika mada ya Ufundishaji. Walitumia maarifa na ujuzi huo kueleza kwa ufasaha mbinu zinazoweza kutumika kufundishia na kujifunzia dhana ya "Uimbaji wa solfa". Mbinu zilizoelezwa na watahiniwa hao ni pamoja na: *mbinu ya bungua bongo, maswali na majibu, mbinu ya majadiliano, ziara, mbinu ya kualika mgeni* na *onesho mbinu*. Hata hivyo, baadhi ya watahiniwa katika kundi hili walishindwa kupata alama zote 4 kwa sababu hawakuweza kutoa maelezo ya kutosheleza katika baadhi ya hoja walizotaja. Kielelezo Na. 8.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.


8 Mbinu (4) zinazoweza kutumika kufundisha-
na kujifunza dhana ya Uimbaji wa Solfa:-
(i) Mbinu ya maswali na majibu; mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi maswali mbalimbali kuhusu Uimbaji wa Solfa.

(ii) Mbinu ya majadiliano; vile vile mwalimu anaweza kuwaongoza wanafunzi wajadiliane kuhusu chochote wanachokiju-
a kuhusu uimbaji wa solfa.


(iii) Ziara; mwalimu anaweza kuandaa
ziara ya kutembelea vikundi mbalim
bali vya kwaya na waimbaji wengi-
ne na kujifunza kuhusu uimbaji
wa solfa.


(iv) Mbinu ya kumualika mgeni; vilevile
mwalimu anaweza kumualika mtu
au mtaalamu wa muziki mfano-
waalimu wa kwaya na kuwaeleke-
za wanafunzi kuhuvu uimbaji-
wa solfa.

**Kielelezo Na. 8.1:** *Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 8..*

Katika Kielelezo Na. 8.1, mtahiniwa aliweza kueleza kwa ufasaha mbinu zinazoweza kutumika kufundishia na kujifunzia dhana ya uimbaji wa solfa.

Watahiniwa waliopata kuanzia alama 2 hadi 2.5 walitoa maelezo ambayo hayakujitosheleza katika hoja walizotaja. Watahiniwa wengine walitaja mbinu sahihi lakini hawakutoa maelezo yoyote kinyume na swali lilivyotaka. Vilevile, watahiniwa wachache waliweza kueleza hoja mbili tu kwa usahihi wakati nyingine mbili hazikuwa sahihi.

Kwa upande mwingine, wengi wa watahiniwa waliopata ufaulu hafifu, walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya Ufundishaji, hivyo kuandika mambo ambayo hayahusiani na mbinu za kufundishia na kujifunzia. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika: *kuteua kundi la wasichana sauti ya kwanza, kuteua kundi la wasichana sauti ya pili, kuteua kundi la wavulana sauti ya tatu* na *kuteua kundi lingine la wavulana sauti ya nne*. Majibu haya yalionekana kutoendana na mahitaji ya swali. Mtahiniwa mwingine aliandika hoja zifuatazo: *mbinu ya matendo, mbinu ya maneno, mbinu ya maandishi* na *mbinu ya ishara*. Kielelezo Na. 8.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kutoa hoja sahihi katika swali hili.



8. i. Kuteua Kundi la wasichana sauti ya Kwanza
ii Kuteua Kundi la wasichana sauti ya pili
iii Kuteua Kundi la wavulana sauti ya latu
iv Kuteua Kundi la wavulana sauti ya nne.

**Kielelezo Na. 8.2:** *Sampuli ya jibu ambalo sio sahihi katika swali la 8.*

Katika Kielelezo Na. 8.2, mtahiniwa aliandika makundi ya waimbaji badala ya mbinu zinazoweza kutumika kufundishia na kujifunzia dhana ya "Uimbaji wa solfa".


### 2.1.9 Swali la 9: Usanii wa picha, chapa, maumbo na mapambo

Swali lilimtaka mtahiniwa kutaja faida nne atakazozipata mwanafunzi kwa kujifunza fani ya utengenezaji wa mapambo mbalimbali. Jumla ya watahiniwa 4,201 (100%) walifanya swali hili. Miongoni mwao, watahiniwa 3,737 (89.0%) walipata kuanzia alama 3 hadi 4, watahiniwa 364 (8.6%) walipata kuanzia alama 2 hadi 2.5 na wengine 100 (2.4%) walipata kuanzia alama 0 hadi 1.5. Kiwango cha kufaulu katika swali hili ni kizuri kwani watahiniwa 4,101 (97.6%) walipata kuanzia alama 2 hadi 4. Kiwango cha kufaulu katika swali hili kimeoneshwa kwenye Chati Na. 6.




**Chati Na. 6:** *Kufaulu kwa watahiniwa katika swali la 9.*

Watahiniwa wengi waliokuwa na ufaulu mzuri waliweza kutaja kwa usahihi faida atakazozipata mwanafunzi kwa kujifunza fani ya utengenezaji wa mapambo mbalimbali. Waliweza kutoa hoja, kama vile: *kupata ajira binafsi*, *kukuza kipato chake*, *kufahamika na kujitangaza kibiashara*, *kukuza kipaji chake*, *kukuza pato la Taifa* na *kuajiri watu wengine*. Watahiniwa hao walionesha kuwa na maarifa ya kutosha katika mada hii na waliweza kutoa maelezo yaliyokidhi matakwa ya swali. Kielelezo Na. 9.1 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.


9 i) Kupata ujuzi wa kutengeneza mapambo
ii) Kujipatia kipato baada ya kutengeneza na
kuuza mapambo yake.
iii) Kupata ajira. Mfano: ajira ya kutengeneza na
kuuza mapambo na kupamba kumbi.
iv) Kuingiza kipato kwenye serikali: kutokana na
kununua na kuuza mapambo atatoa ushuru ambao
huinua kipato cha nchi.


**Kielelezo Na. 9.1:** *Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 9.*

Katika Kielelezo Na. 9.1, mtahiniwa aliweza kubainisha kwa usahihi faida atakazozipata mwanafunzi kwa kujifunza fani ya utengenezaji wa mapambo mbalimbali.

Watahiniwa waliopata ufaulu wa wastani (kuanzia alama 2 hadi 2.5) waliandika hoja sahihi na ambazo sio sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa faida sahihi mbili, kisha akaandika: *kutafuta sifa na kujionyesha* na *kuwa na stadi ya ubunifu*, ambazo sio sahihi. Mtahiniwa mwingine aliandika: *mwanafunzi huweza kutumia maarifa hayo katika maisha* yake na *mwanafunzi huvutiwa na somo na kumpenda mwalimu wa somo la stadi za kazi*.

Kwa upande mwingine, wengi wa watahiniwa waliopata ufaulu hafifu katika swali hili, ilitokana na kushindwa kuelewa matakwa ya swali. Kwa mfano, baadhi ya watahiniwa walitaja fani mbalimbali za kisanaa, kama vile: *fani ya ususi, upambaji*, *uchoraji, uchongaji, fani ya utengenezaji maumbo, fani ya kupangilia rangi vizuri, ususi, ufumaji* na *ushonaji*. Watahiniwa wengine walionesha kukosa maarifa ya kutosha katika mada

hii, hivyo walitaja majibu yasiyohusiana na swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika: *huongeza ari ya kujifunza, huondoa woga kwa kufanya kazi kwa vitendo, humfanya kufikiri zadi* na *huweza kufanya shughuli nyingi za sanaa za maonyesho kwa wakati mfupi*, majibu ambayo sio sahihi. Kielelezo Na. 9.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyepata ufaulu hafifu katika swali hili.



9 ·Faida nne atakazopata Mwanafunzi kwa kujifu
nza fani ya utengenezaji wa mapambo mbalimbali
1· fani ya upambaji
2· fani ya uchongaji
3· fani ya ufumaji
3· fani ya uchoraji

**Kielelezo Na. 9.2:** *Sampuli ya jibu ambalo sio sahihi katika swali la 9.*

Katika Kielelezo Na. 9.2, mtahiniwa alitaja mifano ya fani za sanaa badala ya faida za kujifunza fani ya utengenezaji wa mapambo.


### 2.1.10 Swali la 10: Ufundishaji

Swali lilimtaka mtahiniwa kubainisha hasara nne zinazoweza kujitokeza iwapo mbinu ya majadiliano haitaandaliwa ipasavyo katika kufundishia na kujifunzia somo la Stadi za Kazi. Kati ya watahiniwa 4,201 (100%) waliofanya swali hili, 3,776 (89.9%) walipata kuanzia alama 3 hadi 4 na 356 (8.5%) walipata kuanzia alama 2 hadi 2.5. Watahiniwa wengine 69 (1.6%) walipata kuanzia alama 0 hadi 1.5. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa wa kiwango kizuri kwani watahiniwa 4,132 (98.4%) walipata kuanzia alama 2 hadi 4. Kiwango cha kufaulu katika swali hili ni kama inavyoonekana kwenye Chati Na. 7.




**Chati Na. 7:** *Kufaulu kwa watahiniwa katika swali la 10.*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa umeonesha kuwa watahiniwa waliofanya swali hili vizuri walionesha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya mbinu za ufundishaji. Walielewa kuwa endapo mbinu ya majadiliano haitaandaliwa ipasavyo katika kufundishia na kujifunzia somo la Stadi za Kazi, yafuatayo yanaweza kujitokeza: *muda mwingi huweza kupotea kwa majadiliano marefu, mwenyekiti asipokuwa makini washiriki huweza kujadili mambo yaliyo nje ya mada, huweza kugeuka kuwa mhadhara pale mtu mmoja anapomiliki mazungumzo, wanafunzi huweza kushindwa kuielewa mada husika, kelele na mabishano huweza kutokea* na *inaweza kuwavunja moyo wanafunzi wazito endapo hawatapewa nafasi ya kushiriki katika vikundi vya majadiliano*. Kielelezo Na. 10.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kujibu kwa usahihi swali hili.



10. i/ Huweza kuwapotosha wanafunzi kuhusiana na jambo wanalojifunza
ii/ Huweza kusababisha kelele na mabishano miongoni mwa wanafunzi.
iii/ Huweza kutumia muda mrefu kukamilika-kwa sababu ya maandalizi hafifu mabovu.
iv/ Hupelekea wanafunzi kushindwa kuelewa vizuri mada inayojadiliwa kwa sababu ya matayarisho mabovu.

**Kielelezo Na. 10.1:** *Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 10.*

Katika Kielelezo Na. 10.1, mtahiniwa aliweza kubainisha kwa usahihi hasara zinazoweza kujitokeza iwapo mbinu ya majadiliano haitaandaliwa ipasavyo katika kufundishia na kujifunzia somo la Stadi za Kazi.

Aidha, watahiniwa waliopata ufaulu wa wastani walitoa hoja mbili tu ambazo ni sahihi. Watahiniwa hao waliandika hoja nyingine ambazo sio sahihi, kama vile: *kumjengea mwanafunzi uwezo wa kujieleza, kuleta matabaka baina ya wanafunzi, mwalimu kutumia nguvu nyingi katika kuelekeza, kutokea kwa ajali na kelele nyingi, inakuwa vigumu kutathmini* na *humwezesha mwanafunzi kuongea kwa sauti kubwa.*

Hata hivyo, watahiniwa wachache (1.6%) walishindwa kujibu vizuri swali hili kutokana na kukosa maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya mbinu za ufundushaji. Hali hii ilipelekea kuandika hoja ambazo hazikuwa na uhusiano na swali, kama vile: *kupoteza udadisi, mwalimu kutumia nguvu nyingi kuelekeza, walimu kuchoka sana, mwalimu kushindwa kufundisha, wanafunzi kuchoka, wanafunzi kutoroka kipindi, kufundisha kwa mabishano katika vikundi, kuleta matabaka baina ya wanafunzi* na *mbinu hii haikuzi kipaji cha mwanafunzi*. Kielelezo Na. 10.2. ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili vibaya.


10 (i) Kupoteza udadisi

(ii) Mwalimu kutumia nguvu nyingi katika kueleleza /kufundisha

(iii) Kufundisha kwa Mabishano katika kikundi

(iv) Kuleta matabaka baina ya Wanafunzi

**Kielelezo Na. 10.2:** *Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 10.*


Katika Kielelezo Na. 10.2, mtahiniwa alijibu swali hili vibaya kwani hoja alizotoa hazikukidhi matakwa ya swali, hivyo akapata ufaulu hafifu.

## 2.2 SEHEMU B

Sehemu B ya mtihani huu ilikuwa na maswali 3 (swali la 11 hadi 13) ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali 2 tu. Kila swali lilikuwa na alama 15. Viwango vya kufaulu kwa kila swali vilikuwa kama ifuatavyo: Ufaulu mzuri ulianzia alama 10.5 hadi 15, ufaulu wa wastani ulianzia alama 6 hadi 10 na ufaulu hafifu ulianzia alama 0 hadi 5.5.


### 2.2.1 Swali la 11: Sanaa za Maonyesho

Swali lilimtaka mtahiniwa kufafanua fani sita zinazopatikana katika sanaa za maonyesho. Jumla ya watahiniwa 2,858 (68.0%) kati ya 4.202 waliofanya mtihani huu walichagua swali hili. Uchambuzi wa takwimu umeonesha kuwa watahiniwa 1,048 (36.7%) walipata alama 0 hadi 5.5, watahiniwa 1,007 (35.2%) walipata kuanzia alama 6 hadi 10 na wengine 803 (28.1%) walipata kuanzia alama 10.5 hadi 15. Kwa ujumla, ufaulu wa watahiniwa ulikuwa wa kiwango cha wastani kwani watahiniwa 1,810 (63.3%) walipata alama 6 na zaidi. Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili ni kama inavyoonekana kwenye Chati Na. 8.




**Chati Na. 8:** *Kufaulu kwa watahiniwa katika swali la 11.*

Watahiniwa waliopata alama 10.5 hadi 15 waliweza kufafanua kwa usahihi fani sita zinazopatikana katika sanaa za maonyesho. Walielezea kwa kifupi fani za: *maigizo*, *ngoma za asili au za kisasa*, *kughani mashairi*, *majigambo*, *masimulizi ya hadithi*, *ngonjera* na *uimbaji wa nyimbo*. Watahiniwa hao walidhihirisha kuwa na maarifa ya kutosha kwani pamoja na kufafanua kwa usahihi fani walizozitaja, waliandika utangulizi na hitimisho linalohusiana na swali. Kielelezo Na. 11.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.


11. Sanaa za maonyesho, ni sanaa ambazo hutumika kutambulisha utamaduni wa jamii fulani kupitia kazi zake za kisanaa. Sanaa za maonyesho huweza kuwa kitambulisho kizuri cha utamaduni wetu wa kitanzania. Zifuatazo ni fani zinazopatikana katika sanaa za maonyesho.

Maigizo, kupitia sanaa zetu tunaweza kupata maigizo mbalimbali yenye mafunzo mengi kuhusu tamaduni zetu na kutuelimisha. Maigizo hayo huweza kufanyika katika majukwaa au katika kupitia sauti za wahusika wa igizo hilo.

11. Ngoma za asili, katika maonesho tunaweza kutambulisha utamaduni wetu kupitia ngoma za asili ambapo huwa na wachezaji wa ngoma, wapigaji wa ngoma na ala za muziki huweza kutumika ili ngoma ziwe kuvutia watazamaji.

Kughani mashairi, pia katika sanaa za maonesho tunaweza kughani mashairi mbalimbali ambayo huweza kutambulisha utamaduni wetu wa kitanzania. Mashairi hayo huweza kuonyesha mbele ya hadhira au kupitia machapisho mbalimbali na kusikika redioni.

Uimbaji wa nyimbo, nyimbo katika sanaa huweza kutumika ili kuleta ujumbe kuhusu jambo fulani kupitia kikundi cha watu wanaoimba nyimbo hizo ambapo nyimbo hizo huweza kuimbwa katika majukwaa mbalimbali ya kisanaa au la.

Majigambo hii ni kazi ya sanaa ambayo hutumika ili kukisifia kitu kwa uzuri wake mfano uzuri wa nchi ya Tanzania na rasilimali zake. Fani hii huweza kutumika katika mikutano mbalimbali yenye watu kutoka mataifa mbalimbali ili ~~kusi~~ kusifu uzuri wa Tanzania.

Masimulizi ya hadithi mbalimbali hii pia ni fani inayoweza kupatikana sanaa za maonesho kupitia fanani mbalimbali katika kazi ya sanaa. Masimulizi haya huweza kuwa kuhusu historia ya jambo fulani katika jamii au nchi.

Hivyo basi, sanaa za maonesho ni muhimu katika ukuaji wa sanaa yetu ambapo huleta mabadiliko chanya katika jamii yetu. Pia sanaa za maonyesho zimeweza kuinua vipaji vya watu mbalimbali kupitia kazi za sanaa.

**Kielelezo Na. 11.1:** *Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 11.*

Katika Kielelezo Na. 11.1, mtahiniwa aliweza kufafanua kwa usahihi fani zinazopatikana katika sanaa za maonyesho.

Aidha, watahiniwa waliopata ufaulu wa wastani wa alama 6 hadi 10 walitoa maelezo ambayo hayakujitosheleza katika baadhi ya hoja. Watahiniwa wengine waliweza kufafanua kwa usahihi fani tatu hadi nne na hivyo kuandika hoja mbili hadi tatu ambazo hazikuwa sahihi. Baadhi ya watahiniwa walishindwa pia kuandika utangulizi na hitimisho lisilohusiana na matakwa ya swali, hivyo wakashindwa kupata alama nzuri.

Kwa upande mwingine, watahiniwa wengi waliopata alama 0 hadi 5.5 walikosa maarifa ya kutosha katika mada ya Sanaa za maonyesho. Pia walikosa uelewa wa kutosha katika stadi ya kujibu maswali ya insha. Kwa mfano, baadhi ya watahiniwa waliandika fani mbalimbali za sanaa nyingine, kama vile: *uchoraji*, *uchongaji*, *mapambo*, *utungaji*, *uundaji*, *ususi*, *ufinyanzi*, *ushonaji* na *michezo* badala ya fani zinazopatikana katika sanaa za maonyesho. Watahiniwa wengine walishindwa kuelewa matakwa ya swali hili. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alielewa neno "fani" kama "sifa". Kwa hiyo, alifafanua sifa za sanaa za maonyesho badala ya kueleza aina zake ambapo aliandika: *wahusika*, *mandhari*, *ujumbe*, *falsafa*, *mtindo* na *muundo*. Kielelezo Na. 11.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyepata ufaulu hafifu katika swali hili.

| | |
|---|---|
| 11 | Sanaa za maonyesho ni ufundi unaotumika katika |
| | kuzuwelea hadharani kani mbalimbali zilizofanywa mbele |
| | la mkusanyiko wa watu kwa lengo la kuzionyesha - |
| | ili kama kutazamwa na nguso na kuzitaka kazi hizo |
| | ziwe kununuliwa mfano wa Sanaa za maonesho |
| | ni Uchongaji, uchoraji, uimbaji, ususi, ufinyanzi. Zote |
| | atazo ni fani fani Sita zinazopatikana katika - |
| | Sanaa za Maonyesho. |
| | Uchongaji, ni fani ambayo inahusisha utengenezaji - |
| | wa Vitu mbalimbali kwa nyia ya kuchonga. kwa kutu- |
| | mia mbao au miti. Mfano, uchongaji wa Vinyago, |
| | Vigoda, Sanamu ambazo hutumika katika Sanaa za |
| | maonyesho, watu huvutiwa na kuhitaji kazi hizo. |

11 Uchoraji ni fani inayohusiana na matumizi ya vipande mbalimbali vya mistari vinavyounganishwa kwa pamoja na hatimaye kuleta taswira halisi ya kitu, mfano, Uchoraji wa picha za vitu, michoro au picha za wanyama, mazingira ya dunia, binadamu pamoja na mambo yanayomzunguka binadamu. Picha, michoro ya aina mbalimbali hutumika kama Sanaa za Maonyesho.

Ufinyanzi; ni mchakato wa kuunda kitu kwa kutumia udongo wa mfinyanzi, ambao matokeo yake huwezesha kupatikana kwa vitu kama vile, vyungu, mitungi, kwa matumizi mbalimbali kupikia na kuhifadhia maji. Vitu hivi hutumika kama Sanaa za maonyesho.

Ushonaji; hii ni fani ambayo inahusiana na uunganishaji wa vitambaa kwa kutumia uzi. fani hii inawezesha kupatikana kwa mitindo ya nguo mbalimbali, kutegemeana na ufundi utumikao. Mitindo hiyo ya nguo hutumika katika Sanaa za maonyesho.

Ususi; ni fani ambayo inahusiana na upishanishaji wa chani za miti na kupata kitu fulani mfano, mkeka, kikapu. Ambavyo huwa ni Sanaa za Maonyesho, watu mbalimbali huvienda na kutazama wanapovutiwa hununua Sanaa hizo


Sanaa za Maonyesho ni muhimu kwa sababu zinahusiana na kudumisha Utamaduni, pamoja na kukuza uchumi wenye kusababisha kuwepo kwa vitu mbalimbali vyenye matumizi tofautitofauti, na kuwa chanzo cha uwezo wa watu katika kudadisi na kutatua au kupata majibu kuongezeka

**Kielelezo Na. 11.2:** *Sampuli ya jibu ambalo sio sahihi katika swali la 11.*

Katika Kielelezo Na. 11.2, mtahiniwa alifafanua fani zinazopatikana kwenye sanaa nyingine badala ya fani zinazopatikana katika sanaa za maonyesho.

### 2.2.2 Swali la 12: Ushoni wa Nguo

Swali lilimtaka mtahiniwa kuchambua aina tano za mishono ya kutumia mikono na kuonesha kazi ya kila mshono. Jumla ya watahiniwa 1,380 (32.8%) walichagua swali hili. Miongoni mwao, watahiniwa 768 (55.7%) walipata kuanzia alama 10.5 hadi 15, watahiniwa 364 (26.3%) walipata kuanzia alama 6 hadi 10 na watahiniwa 248 (18.0%) walipata kuanzia alama 0 hadi 5.5. Watahiniwa 1,132 (82.0%) walipata kuanzia alama 6 hadi 14.5, hivyo kiwango cha kufaulu katika swali hili kilikuwa ni kizuri. Chati Na. 9 inaonesha kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili.




**Chati Na. 9:** *Kufaulu kwa watahiniwa katika swali la 12.*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa umeonesha kuwa watahiniwa waliopata ufaulu mzuri katika swali hili walikuwa na maarifa ya kutosha yaliyowawezesha kuelewa kwa ufasaha mahitaji ya swali. Watahiniwa hao waliweza kuchambua kwa usahihi aina tano za mishono ya nguo ya kutumia mikono ambayo ni pamoja na hii ifuatayo: *mshono wa pindo*, *mshono wa kurudia*, *mshono mshikizo*, *mshono wa blanketi* na *mshono shuru*. Waliweza pia kutoa kazi ya kila mshono waliotaja. Watahiniwa hao, pia walionesha kuwa na stadi ya kuandika insha kwani waliweza kutoa utangulizi na hitimisho lililojitosheleza. Kielelezo Na. 12.1 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.

12. Mishono sahili: Ni kitendo cha kutengeneza nguo kwa kutumia mshono rahisi wa kitambaa pamoja na vifaa vya ushonaji kwa kutumia stadi ya kushona binadamu ameweza kujikuamu kimaisha kutoka hali ya umaskini na kuwa na hali nzuri kimaisha kwa kushona.


Zipatazo ni aina za kushona kwa kutumia mikono na kazi zake.

Mshono wa pindo: Huu ni mshono wa aina inayohusika na kupinda kitambaa na kuunganisha kwa kupinda sehemu za pembeni. Kazi hii hufanyika mara nyingi kwenye nguo kama kanga, vitenge kwa kupinda baada ya kukata.

Mshono wa kurudiarudia: Ni aina ya ushonaji kwa kushona mara kwa mara sehemu iliyoshonwa ili kuifanya sehemu hiyo isiachie. Pia husaidia kuepuka kupumuka kwa nguo hiyo.

Mshono wa mshikizo: Ni kitendo cha kuunganisha vitambaa viwili au zaidi ili kutengeneza nguo. Mshono huu huhusika na kuongeza kitambaa na kufanya vazi. Pia kushikiza sehemu zilizopumuka ili kuweka uimara katika vazi.

Mshono wa blanketi: Ni kitendo cha kupamba nguo na kuondoa nyuzi za vazi kwenye kitambaa ili kuifanya kuwa na nadhifu zaidi. Pia uwekaji huu katika nguo ni kufanya vazi lipendeze na kuonekana bora zaidi.


Mshono shuni: Ni aina ya mshono sahihi ambao hutumika kutengeneza kazi kwa kuunganisha vitambaa. Mshono huu husaidia kupata mavazi mbalimbali kwa kutu mia kuunganisha.
Kwa ujumla mishono ya kutumia mikono ipo mitano ambayo husaidia upatikanaji wa mavazi, unadhifu katika mavazi na pia kusaidia jamii au wajasiriamali kupata kipato kwa kutengeneza nguo.

**Kielelezo Na. 12.1:** *Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 12.*

Katika Kielelezo Na. 12.1, mtahiniwa aliweza kuchambua kwa usahihi aina tano za mishono ya kutumia mikono na kuonesha kazi za kila mshono.

Watahiniwa waliopata ufaulu wa wastani walionesha kukosa maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya aina za mishono. Baadhi yao walishindwa kutoa maelezo yanayotosheleza wakati wengine walichambua hoja pungufu. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja pamoja na kuelezea hoja mbili kwa usahihi na kuandika utangulizi na hitimisho linaloendana na matakwa ya swali, alielezea pia hoja tatu ambazo hazikuwa sahihi kwa kuandika: *mshono wa mabanda mafupi*, *mshono wa mabanda marefu* na *mshono wa kunyonga*.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 248 (18.0%) walipata ufaulu hafifu kutokana na sababu mbalimbali. Baadhi yao walishindwa kuelewa matakwa ya swali ambapo walieleza aina za mishono ya kutarizi au kudarizi kwa kutumia mikono, kama vile: *mshono wa mwiba wa samaki, mshono wa zigizaga, mshono wa mnyororo, mshono wa kokoto* na *mshono wa msalaba* badala ya mishono ya kushona nguo kwa kutumia mikono. Watahiniwa wengine hawakuwa na ujuzi na maarifa ya kutosha kuhusu makundi, mifano na matumizi ya mishono ya kushona nguo. Watahiniwa hao walielezea aina za mishono ya nguo za wanawake, kama vile: *mshono wa nguva, solo, mapande sita, rinda boksi, marinda ya kuvuta, marinda ya kufukuzana, kimini* na *taiti*. Watahiniwa wengi katika kundi hili, pia walishindwa kuandika utangulizi na hitimisho linalohusiana na swali. Kielelezo Na. 12.2 kinaonesha sampuli ya jibu toka kwenye skripti ya mtahiniwa aliyepata ufaulu hafifu.

12 Mishono ni mitindo mbalimbali ya ubunifu ambayo mtu hutumia katika kushona mavazi mbalimbali. Kila aina ya mavazi yana mshono wake maalumu mfano mshono wa polisi unatofautiana na mishono mingine. Ifuatayo ni aina za mishono ya kutumia mikono mishono hiyo ni kama vile:-


Mshono wa solo kwa mwanamke. Mshono huu ni aina ya mshono ambayo hutumiwa na wanawake kwa ajili ya kuwapendezesha. Baadhi ya wanawake hupenda mshono huu kwa sababu ni mshono mzuri.

Mshono wa linda boksi, hii ni aina ya mshono ambayo hutumiwa kwa asilimia kubwa na police (trafiki) kama ndio mshono wa sale zao za nguo za kazi lakini pia mshono huu hutumiwa na wanafunzi wa sekondari na vyuo vya kati kama sale za kusomea

Mshono wa nguva, hii nayo ni aina ya mishono ambayo nayo hutumiwa na wanawake kwa asilimia kubwa. Hushona nguo zao na kutokea lakini pamoja na za kushi ndia majumbani mwao

Mshono wa mapande sita, pia hii nayo ni aina ya mshono ambayo hupenda kushona wanawake katika mavazi ~~mb~~ mbalimbali ya nguo zao lengo la mshono huu ni kupendeza na kuwa na muonekano mzuri katika jamii inayo mzunguka.

Mshono wa malinda mawili, pia hii nayo ni aina ya mishono ambayo hupendwa


Mshono wa nguva, hii nayo ni aina ya mishono ambayo nayo hutumiwa na Wanawake kwa asilimia kubwa. Hushona nguo zao na kutokea lakini pamoja na za kushindia majumbani mwao

Mshono wa Mapande Sita, pia hii nayo ni aina ya mshono ambayo hupenda kushona wanawake katika mavazi ~~mb~~ mbalimbali ya nguo zao lengo la mshono huu ni kupendeza na kuwa na muonekano mzuri katika jamii inayo mzunguka.

Mshono wa Mahinda mawili, pia hii nayo ni aina ya mishono ambayo hupendwa katika umuhimu huo.

**Kielelezo Na. 12.2:** *Sampuli ya jibu ambalo sio sahihi katika swali la 12.*

Katika Kielelezo Na. 12.2, mtahiniwa alifafanua aina za mishono ya nguo ya akina mama badala ya mishono ya kutumia mkono. Mtahiniwa huyu pia aliandika utangulizi na hitimisho lisilohusiana na swali.

### 2.2.3 Swali la 13: Kilimo, ufugaji na uvuvi

Swali lilimtaka mtahiniwa kueleza faida sita za kufuga wanyama. Jumla ya watahiniwa 4,148 (98.7%) kati ya watahiniwa 4,202 waliofanya mtihani huu walichagua swali hili. Miongoni mwao, watahiniwa 3,859 (93.0%) walipata kuanzia alama 10.5 hadi 14.5 na 288 (7.0%) walipata kuanzia alama 6 hadi 10. Hata hivyo, ni mtahiniwa 1 tu alikuwa na ufaulu hafifu kwa kupata alama 1.5. Kiwango cha kufaulu katika swali hili kilikuwa ni kizuri kwani watahiniwa 4,147 (100%) walipata alama 6 na zaidi kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 4.

| Alama | Asilimia ya Watahiniwa |
|---|---|
| 0 – 5.5 | 0.0 |
| 6 – 10 | 7.0 |
| 10.5 - 15 | 93.0 |

**Jedwali Na. 4**: *Kufaulu kwa watahiniwa katika swali la 13.*

Watahiniwa waliopata alama 10.5 hadi 14.5 waliweza kueleza kwa ufasaha faida za kufuga wanyama, kama vile: *hutupatia kipato*, *hutupatia kitoweo/chakula kama nyama, mayai na maziwa*, *hutupatia mbolea/samadi inayotusaidia kuboresha kilimo na ustawishaji wa mazao*, *husaidia kuinua uchumi wa taifa kwa kulipa kodi*, *ni chanzo cha ajira*, *wanyama hutumika katika kilimo na kubeba mizigo*, *baadhi ya wanyama hutumiwa katika ulinzi wa majumbani na maeneo mengine* na *kupata mazao kama ngozi ambazo hutumika kutengeneza bidhaa mbalimbali*. Majibu hayo yalidhihirisha watahiniwa kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya ufugaji na uwezo wa kuhusianisha maarifa waliyopata darasani na matumizi ya mazao mbalimbali yanayotokana na shughuli za ufugaji zinazofanyika katika jamii wanamoishi. Watahiniwa hao, pia walikuwa na stadi ya kuandika insha kwani waliandika utangulizi na hitimisho linaloendana na matakwa ya swali. Kielelezo Na. 13.1 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.

13. Wanyama ni jumla ya viumbe hai wote ambao wapo kwenye kundi la mamalia. Wanyama hawa wanaweza kuwa wanyama wa porini au wanyama wanaofugwa na binadamu. Wanyama wanaofugwa na binadamu ni wale ambao mwanadamu huwafuga kwa ajili ya kazi mbalimbali mfano katika kazi za kilimo, kazi za ulinzi na pia kwa ajili ya kupata mbolea. Mfano wa wanyama wanaofugwa na binadamu ni pamoja na Ng'ombe, Mbuzi, Kondoo, Mbwa, Sungura Paka na Nguruwe.

Kuna faida kubwa za kufuga wanyama, baadhi ya faida hizo ni:-

Hutupatia Mbolea; Kutokana na ufugaji wa wanyama, tunafaidika kwa kupata mbolea ambazo hutumika shambani kwa ajili ya kuzalisha na kurutubisha ardhi. Wanyama wanaotoa mbolea ni Ng'ombe, Mbuzi, Sungura na Nguruwe na Mbolea hii kwa kitaalamu huitwa Mbolea ya samadi ambayo hutumika zaidi kwenye maeneo ya wafugaji.


13. Hulipatia Kitoweo; Ufugaji wa wanyama pia unasaidia katika upatikanaji wa kitoweo. Lakini wengi hufuga wanyama kwa ajili ya kitoweo. Wanyama - kama vile Sungura mara nyingi wamekuwa wakitumika kama kitoweo kwa mfugaji lakini pia hata wanyama wengine na wao wamekuwa wakitumika katika upatikanaji wa vitoweo katika sehemu mbalimbali. Mfano Buchani.

Hutuingizia kipato; kutokana na ufugaji pia tunaweza kupata kipato cha hali ya juu. Kipato kinapatikana kutokana na uuzaji wa wanyama hao na kupata fedha ambazo zinaweza kutumika katika mahitaji mengine kama vile chakula, mavazi na makazi. Mfano wa wanyama ambao hutuingizia kipato ni pamoja na Ng'ombe ambapo ukiuza ng'ombe watano utakuwa na hela ya kutosha.

Ngozi za wanyama hutumika katika kutengenezea vitu mbalimbali; kupitia wanyama wanaofugwa na binadamu, pia tunaweza kupata ngozi ambazo zinaweza kutumika katika kutengenezea vitu mbalimbali kama vile viatu, mikanda pamoja na mabegi ya aina mbalimbali.

Hutusaidia katika shughuli za kilimo; kutokana na kufuga wanyama pia inatusaidia katika shughuli za kilimo ambapo wanyama kama vile ng'ombe wamekuwa wakitumika zaidi katika kulima kwa kufungwa kwenye jembe la ng'ombe (Plau) kitu ambacho kimewasaidia wakulima kulima sehemu kubwa kwa gharama nafuu zaidi kuliko kutumia Trekta.

Vilevile hutusaidia katika shughuli za ulinzi nyumbani na kwenye taasisi mbalimbali, kutokana na ufugaji wa mbwa pia imesaidia kuwepo na hali ya usalama na amani katika jamii zetu hasa kwa wakulima na wafugaji ambapo mbwa wamekuwa wakilinda na kuzuia hatari kama vile wizi pamoja na wanyama wakali kuja kuchukua ng'ombe na mbuzi.



13 Kutokana na faida hizo, lakini pia ku
na mambo ya kuzingatio kabla ya kuanzisha
ufugaji na mambo hayo ni kuwa na chakula cha
kutosha kwa ajili ya wanyama hao, kuwa na vyombo
vya kutosha kwa ajili ya kuwalishia, Malibabu
kwa wanyama lakini pia kuwa ufugaji wa wanyama -
wengi ni lazima upate eneo la kutosha kuwalishia.

**Kielelezo Na. 13.1:** *Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 13.*

Katika Kielelezo Na. 13.1, mtahiniwa aliweza kueleza kwa usahihi faida za kufuga wanyama. Mtahiniwa huyu pia alionesha kuwa na stadi ya kujibu maswali ya insha kwani alitoa utangulizi na hitimisho linaloendana na matakwa ya swali.


Kwa upande mwingine, watahiniwa wachache (7.0%) walipata ufaulu wa wastani katika swali hili kwa sababu walitoa maelezo ambayo hayakujitosheleza katika baadhi ya hoja walizotaja au walitoa hoja pungufu. Walieleza baadhi ya hoja ambazo hazikuwa sahihi, kama vile: *kuonesha ufahari wa familia fulani*, *kuepuka migogoro kati ya wakulima kwa wakulima*, *wanyama hupunguza nyasi na vichaka*, *kuitumia ardhi kwa ubora unaotakiwa*, *kuonesha mfano mzuri katika kufuga* na *kuwa na wanyama wanaokula mabaki ya vyakula*. Kwa nyongeza, watahiniwa wengine katika kundi hili waliichambua hoja moja na kuiandika kama hoja mbili au tatu tofauti. Kwa mfano, *wanyama kutupatia nyama, kutupatia maziwa* na *kutupatia mayai* ziliandikwa na baadhi ya watahiniwa kama hoja tatu tofauti badala ya hoja moja ya *kutupatia vyakula kama nyama, maziwa na mayai*. Majibu ya watahiniwa hawa yanaonesha kuwa hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya ufugaji.

## 2.3 SEHEMU C

Sehemu C ya mtihani huu ilikuwa na maswali 3 (swali la 14 hadi 16) ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali 2 tu. Kila swali katika sehemu hii lilikuwa na alama 15. Viwango vya kufaulu kwa kila swali vilikuwa kama ifuatavyo: Ufaulu mzuri ulianzia alama 10.5 hadi 15, ufaulu wa wastani ulianzia alama 6 hadi 10 na ufaulu hafifu ulianzia alama 0 hadi 5.5.

### 2.3.1 Swali la 14: Misingi ya Kufundisha Somo la Stadi za Kazi

Swali lilimtaka mtahiniwa kueleza umuhimu wa msingi wa utendaji, umakini na udadisi katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Stadi za Kazi kwa kutumia hoja tano. Jumla ya watahiniwa 2,713 (64.6%) walifanya swali hili. Miongoni mwao, watahiniwa 1,301 (48.0%) walipata kuanzia alama 10.5 hadi 14.5, watahiniwa 1,349 (49.7%) walipata kuanzia alama 6 hadi 10 na wengine 63 (2.3%) walipata kuanzia alama 0 hadi 5.5. Kiwango cha kufaulu katika swali hili kilikuwa ni kizuri kwani watahiniwa 2,650 (97.7%) walipata kuanzia alama 6 hadi 14.5. Chati Na. 10 inaonesha kiwango kizuri cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili.





**Chati Na. 10**: *Kufaulu kwa watahiniwa katika swali la 14.*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa umeonesha kuwa watahiniwa waliopata ufaulu mzuri walitumia maarifa waliyokuwa nayo kujibu swali hili kwa usahihi. Waliweza kueleza kwa usahihi umuhimu wa msingi wa utendaji, umakini na udadisi katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Stadi za Kazi kwa kutoa hoja, kama vile: *kutenda kunamfanya mwanafunzi kuweka kumbukumbu ya kudumu ya maudhui azipatazo katika matendo, umakini hufanya somo liwe bora na lenye kuvutia zaidi wanafunzi kujifunza, udadisi humfanya mwalimu na mwanafunzi kuwa wagunduzi katika mchakato mzima wa ufundishaji na ujifunzaji, umakini humfanya mwanafunzi kufuatilia somo kwa ukaribu na kujifunza vizuri* na *kutenda kunamfanya mwalimu kuitawala mada na mwanafunzi kuelewa dhana kwa urahisi*. Walionesha pia uelewa katika kuandika insha kwa kutoa utangulizi na hitimisho lililojitosheleza. Hata hivyo, watahiniwa wengi katika kundi hili walishindwa kupata alama zote 15. Hii ni kwa sababu walitoa maelezo

yasiyotosheleza katika hoja moja hadi mbili au walieleza hoja nne kwa usahihi badala ya tano.

Idadi kubwa ya watahiniwa waliopata ufaulu wa wastani walieleza kwa usahihi hoja mbili hadi tatu kati ya tano zilizotakiwa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja pamoja na kuelezea hoja tatu kwa usahihi, aliandika: *kuchochea maendeleo katika jamii* na *kujipatia ajira kwa kutenda*, ambazo sio sahihi. Watahiniwa wengine walishindwa kutoa maelezo yanayojitosheleza kwa baadhi ya hoja. Kwa mfano, wengi wao waliweza kueleza umuhimu wa utendaji, umakini na udadisi kwa upande wa mwanafunzi katika kujifunza. Hata hivyo, hawakueleza umuhimu wake kwa upande wa mwalimu katika kufundisha.

Kwa upande mwingine, baadhi ya watahiniwa waliopata ufaulu hafifu walishindwa kuelewa matakwa ya swali. Kwa mfano, baadhi ya watahiniwa walidhani kwamba swali liliwataka kueleza umuhimu wa somo la Stadi za Kazi jambo lililowafanya kueleza hoja kama vile: *Somo la Stadi za Kazi huweza kuchochea maendeleo katika jamii*, *mtu aliyesoma Stadi za Kazi huweza kujipatia ajira*, *husaidia kuongeza uchumi wa nchi wanapozalisha mali*, *stadi za kazi hutangaza utamaduni wetu*, *husaidia kuzalisha chakula*, *husaidia kuandaa wataalam mbalimbali*, *somo hili huweza kumfanya mtu kuwa mjasiriamali*, *somo hili huwafundisha wanafunzi sanaa ambazo huongeza ushirikiano* na *pia somo hili huweza kuwasaidia wanafunzi kushiriki kirahisi katika mambo ya kijamii*. Watahiniwa wengine walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha katika mada husika. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika: *hutunza mda*, *husaidia kubuni mambo*, *wanafunzi hupenda somo* na *huepusha makosa*. Mtahiniwa huyu alipata alama za chini kwa sababu alishindwa kutoa maelezo ya kutetea hoja zake. Kielelezo Na. 14.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili vibaya.



14. Somo la Stadi za Kazi ni somo ambalo huweza kufundishwa ili kuweza kumwandaa mwanafunzi kuweza kujitegemea katika maisha ya kila siku. Somo hili lina umuhimu mkubwa sana kwa msingi wa utendaji, umakini na udadisi ufundishaji na ujifunzaji, kama ifuatavyo.

Somo la Stadi za Kazi huweza kuchochea maendeleo katika jamii, kutokana na kuwa na utendaji, umakini na udadisi katika ufundishaji na ujifunzaji kitu au mwanafunzi huweza kubuni na kutengeneza vitu mbalimbali.

Somo hili huweza kujipatia ajira, kutokana na kuhusika na utengenezaji wa vitu mbalimbali kwa vitendo huweza kupelekea mtu kuwa mtendaji wa vitu mbalimbali ambavyo huweza kumsaidia kujipatia ajira.

Somo hili la Stadi za Kazi huweza kumfanya mtu kuwa mjasiriamali, hii ni kutokana na kuweza kujihusisha na kufanya biashara ndogondogo katika eneo fulani kutokana na utendaji, umakini na udadisi katika ufundishaji na ujifunzaji.

Kupunguza umasikini, mtu anapofanya kazi au shughuli mbalimbali kama vile ufundi wa nyumba, uhunzi n.k, hivyo huweza kusababisha kupunguza umaskini katika jamii.

Pia somo hili huweza kuandaa wanafunzi kuwa wataalamu au wajuzi wa kuweza kubuni vitu mbalimbali ambavyo vitaweza kuleta mabadiliko makubwa kwa baadaye.


Msingi wa utendaji, umakini na udadisi katika somo la Stadi za Kazi ni muhimu sana kwa sababu huweza kuleta mabadiliko makubwa ya kijamii.

**Kielelezo Na. 14.1:** *Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 14.*

Katika Kielelezo Na. 14.1, mtahiniwa alieleza umuhimu wa somo la Stadi za Kazi badala ya umuhimu wa msingi wa utendaji, umakini na udadisi katika kufundishia na kujifunzia somo la Stadi za Kazi.

### 2.3.2 Swali la 15: Upimaji

Swali lilimtaka mtahiniwa kuchambua hatua tano za kufanya tathmini ya somo la Stadi za Kazi. Jumla ya watahiniwa 1,703 (40.5%) walichagua swali hili. Uchambuzi wa takwimu za swali hili unaonesha kuwa watahiniwa 1,213 (71.2%) walipata kuanzia alama 10.5 hadi 15, watahiniwa 297 (17.5%) walipata kuanzia alama 6 hadi 10 na waliobaki 193 (11.3%) walipata kuanzia alama 0 hadi 5.5. Hii inaonesha kiwango kizuri cha kufaulu kwani watahiniwa 1,510 (88.7%) walipata kuanzia alama 6 hadi 15. Chati Na. 11 inaonesha kiwango cha kufaulu katika swali hili.




**Chati Na. 11**: *Kufaulu kwa watahiniwa katika swali la 15.*


Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa umeonesha kuwa watahiniwa waliopata ufaulu mzuri walitumia maarifa na ujuzi waliokuwa nao kutoa majibu yaliyokidhi matakwa ya swali hili. Watahiniwa hawa waliweza kuchambua kwa usahihi hatua tano za kufanya tathmini ya somo la Stadi za Kazi ambazo ni: *kuchunguza malengo ya somo, kuchunguza ushiriki au uwezo wa wanafunzi darasani, kupima kiwango cha malengo ya somo kilichofikiwa, kusahihisha mazoezi, kutoa alama na kuchunguza matokeo ili kubaini malengo yaliyofikiwa na ambayo hayakufikiwa* na *kuandika matokeo ya tathmini kama malengo yamefikiwa au la*. Watahiniwa hawa, pia walionesha kuwa na stadi ya kutosha ya kujibu maswali ya insha kwani waliweza kuandika hatua zote kwa mtiririko. Kielelezo Na. 15.1 ni sehemu ya sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili vizuri.

15. Tathimini ni kitendo cha kupima na kuchukua data zitakazowezesha katika kufanya maamuzi yatakayowezesha katika urekebishaji na uboreshaji wa masuala mbalimbali katika elimu. Kuna zana za kufanyia tathimini nazo ni mazoezi, mitihani, majaribio, ~~dodos~~ kazi mradi na orodha hakiki. Pia kuna aina za tathimini nazo ni tathimini awali, endelevu, dodoso na tathimini tamati. Zifuatazo ni hatua tano za kufanya tathimini ya somo la stadi za kazi.

Kuchunguza lengo mahsusi la somo ni hatua ya kwanza katika kufanya tathimini ya somo la stadi za kazi. Lengo mahsusi ni ujuzi anaopaswa kupata mwanafunzi ndani ya kipindi husika katika somo husika. Kwa mfano kufahamu aina za usufi. Hivyo katika tathimini lazima kutathimini lengo la somo linahitaji nini na kama limefikiwa. Kwa hiyo ni hatua moja wapo na ya kwanza katika kufanya tathimini ya somo la stadi za kazi.

Kuchunguza ushiriki pamoja na uwezo wa wanafunzi katika kujipima. Pia ni hatua nyingine katika kufanya tathimini ya somo la stadi za kazi. Ushiriki na uwezo wa wanafunzi ni jinsi wanafunzi hujituma na kushiriki katika kujipima. Kwa mfano katika kujibu maswali, kuuliza, kudadisi na kufikiri. Hivyo ~~ufaga~~ tathimini itafanyika kwa kuchunguza uwezo wao katika kujipima ubora. Kwa hiyo ni hatua nyingine katika kufanya tathimini ya somo la stadi za kazi.

Kutoa zoezi au mazoezi yanayoendana na lengo mahususi. Pia ni hatua nyingine katika kufanya tathimini kwa kutoa zoezi kwa wanafunzi linaloendana na lengo mahususi ili kuweza kutathimini somo. Zoezi ni kazi anayopewa mwanafunzi baada ya kujipima lengo husika. Kwa mfano kuna aina ngapi za usufi? Hivyo swali litawezesha kufanya tathimini ya somo kwa kutoa zoezi. Kwa hiyo ni moja wapo ya hatua ya kufanya tathimini ya somo la stadi za kazi.



15. Kusahihisha zoezi na kutoa alama, ili kugundua changamoto walizonazo. Pia ni hatua nyingine katika kufanya tathimini ya somo la Stadi za kazi. Kusahihisha zoezi ni kutagua kazi iliyofanywa na kuisahihisha kisha kutoa alama, hii husaidia kugundua wangapi hawajaelewa na wapi wameelewa. Kwa Mfano Anna kapata 10/10 vizuri au wanafunzi wote wamepata 10/10 vizuri. Kwa hiyo ili kufanya tathimini ya somo hatua nyingine ni kusahihisha zoezi lililotolewa katika somo la stadi za kazi.

Kufanya tathimini ya somo.

Pia ni hatua ya mwisho kabisa katika kufanya tathimini ya somo la stadi la kazi. Tathimini ya somo ni kutathimini somo limeendaje. Kwa mfano kuangalia matatizo yaliyojitokeza na kuyatatua changamoto zilizopatikana na kuzitatua, katika


**Kielelezo Na. 15.1:** *Sampuli ya sehemu ya jibu sahihi katika swali la 15.*

Katika Kielelezo Na. 15.1, mtahiniwa aliweza kuchambua hatua tano za kufanya tathmini ya somo la Stadi za Kazi.

Watahiniwa wengi waliopata ufaulu wa wastani walitaja baadhi ya hoja kwa kubahatisha, hivyo kutoa hatua za kufanya tathmini ya somo la Stadi za Kazi ambazo hazikuwa sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika: *kukusanya data za kuandika ripoti ya wanafunzi* na *kutafuta walengwa wa kufanyiwa tathmini*, ambazo sio hatua sahihi. Watahiniwa wengine waliandika baadhi ya hatua za kufanya tathmini bila kufuata mpangilio unaotakiwa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika hatua ya kwanza ni *kuchunguza uwezo wa wanafunzi* na ya pili *kuchunguza malengo ya somo*. Hali hii ilipelekea kushindwa kupata alama katika hoja hizi.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa umeonesha kuwa baadhi ya watahiniwa waliopata ufaulu hafifu walishindwa kuelewa matakwa ya swali. Watahiniwa hawa walitoa hoja zisizohusiana na matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika: *kutambua tatizo, kuandika au kuandaa mswada, kuandaa zana za utafiti, kukusanya, kuchambua na kutafsiri data* na *kuandika ripoti ya utafiti.* Mtahiniwa huyu alishindwa kuelewa kuwa hizi ni baadhi ya hatua za kufanya utafiti na sio hatua za kufanya tathmini. Mtahiniwa mwingine aliandika aina za tathmini ambapo

alielezea kuhusu *tathmini ya awali, tathmini endelevu, tathmini tamati* na *tathmini tatuzi* kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 15.2.


15 Tathmini ni kitendo cha kujua ni kwa
kiwango gani mwanafunzi anaweze kupata maa
rifa, Stadi na mielekeo mbalimbali ambayo mw
ali wa somo la Stadi za kazi amefundishi.
Hivyo kuna aina tano ambazo zinatumika
katika kutathmini Somo la Stadi za kazi, nazo
ni;
Tathmini ya awali, tathmini hii hufany
wa na Mwalimu kwa kutaka kujua ni ~~kwa~~
kuwa mwanafunzi anaelewa nini au anauf
ahamu kuhusiana na dhana itakayofundishwa
Tathmini endelevu, tathmini hii hufanyw
a na mwalimu mara kwa mara kwa lengo
la kutaka kujua maendeleo ya Mwanaf
unzi wake katika ufundishaji.
Tathmini tamati, tathmini hii ni tathm
ini ya mwisho ambayo mwalimu anaw
eza kutoa maamuzi juu ya tathmini ali
zofanya awali pamoja na endelevu.
Tathmini dadaso, katika tathmini hii
dosari zilizojitokeza katika kufanya tathmi
mi huchunguzwa na kuchambuliwa.
Tathmini tatuzi, dosari zilizojitokeza hu
fanyiwa maamuzi au marekebisho baada
ya kugundua mapungufu yaliyojitokeza.
Hivyo ni nyema Mwalimu kufanya tath
mini la Somo la Stadi za kazi kwani humw
ezesha kujua dosari zinazojitokeza ili kufan
yia marekebisho kabla ya kufundisha.

**Kielelezo Na. 15.2:** *Sampuli ya jibu ambalo sio sahihi katika swali la 15.*

Katika Kielelezo Na. 15.2, mtahiniwa alijibu swali hili kwa kuchambua aina za tathmini badala ya hatua za kufanya tathmini ya somo la Stadi za Kazi.


### 2.3.3 Swali la 16: Maandalizi ya Ufundishaji

Swali lilimtaka mtahiniwa kuonesha umuhimu wa mbinu ya ziara katika kufundishia mada ndogo ya "Matengenezo ya baiskeli" kwa kutumia hoja sita. Jumla ya watahiniwa 3,967 (94.4%) walichagua swali hili. Kati yao, watahiniwa 2,596 (65.4%) walipata kuanzia alama 10.5 hadi 14.5 na 1,366 (34.5%) walipata kuanzia alama 6 hadi 10. Hata hivyo, ni watahiniwa 5 (0.1%) tu ndio walipata kuanzia alama 0.5 hadi 5.5. Watahiniwa 3,962 (99.9%) waliweza kujibu swali hili na kupata alama 6 na zaidi, hivyo kufanya kiwango cha kufaulu kuwa kizuri. Jedwali Na. 5 linaonesha kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa.

| Alama | Asilimia ya Watahiniwa |
|---|---|
| 0 – 5.5 | 0.1 |
| 6 – 10 | 34.5 |
| 10.5 - 15 | 65.4 |

**Jedwali Na. 5:** *Kufaulu kwa watahiniwa katika swali la 16.*

Watahiniwa waliokuwa na ufaulu mzuri katika swali hili (65.4%), walionesha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu umuhimu wa kutumia mbinu ya ziara katika kufundishia mada mbalimbali. Waliweza kuandika hoja sahihi, kama vile: *inawafanya wanafunzi kuwa wenye kujitegemea, humpa nafasi mwanafunzi kuwa katika mazingira halisi wakati wa kujifunza, hufanya dhana ya kutengeneza baiskeli kueleweka kwa kina zaidi, hushirikisha wanafunzi wote, huongeza motisha na kumwezesha mwanafunzi kupenda kujifunza zaidi, huondoa utata unaoweza kuwepo kutokana na mawazo yao ya awali, huwaongezea uwezo wa kujitegemea zaidi kimasomo, huwafanya wanafunzi kuwa wadadisi, ni njia nzuri inayowafanya wanafunzi kujifunza mambo mengi na mwisho kuandika taarifa juu ya ziara waliyofanya, huongeza ushirikiano baina ya wanafunzi na mwalimu katika masuala ya kitaaluma* na pia *inawasaidia wanafunzi kupata taarifa ya kwanza (au ya moja kwa moja) juu ya tukio au dhana fulani badala ya kumtegemea mwalimu*. Watahiniwa hawa pia walionesha kuwa na stadi ya uandishi wa insha kwani waliweza kufuata hatua zote katika kujibu swali hili. Kielelezo Na. 16.1 kinaonesha sampuli ya sehemu ya jibu la mtahiniwa aliyepata ufaulu mzuri katika swali hili.


16. Ziara; Ni mbinu mojawapo kati ya mbinu shirikishi ambayo hufanyika kufundisha wanafunzi. Ni mbinu ambayo wanafunzi huenda kutembelea au kutembelea sehemu fulani mfano Viwandani, Gereji kwa ajili ya kujifunza. Hivyo katika mbinu hii kuna umuhimu wake iwapo mwalimu atawapeleka ziara wanafunzi kujifunza mada ndogo ya Matengenezo ya baiskeli kama ifuatavyo:

Husaidia kujibiwa kwa maswali ya kiufundi ambayo yangekuwa vigumu kwa mwalimu mwenyewe kuyajibu; kutokana na kuwepo fundi mwenyewe hivyo wanafunzi hupata fursa ya kuuliza maswali ya kiufundi zaidi.

Huwafanya wanafunzi kufurahia kutokana na kwenda kujifunzia mazingira tofauti na shule; wanafunzi kwa kawaida hufurahia sana kwenda ziara.

Huwafanya wanafunzi kujifunza kwa vitendo zaidi na kushuhudia kwa macho yao mbali na kuona tu vitabuni. Hivyo huwafanya kuwa na kumbukumbu.

Ziara ikitumika vizuri huwafanya wanafunzi kujifunza na mambo mengine mengi ambayo hata hawakulijengwa hivyo kuwapelekea kujua mambo mengi.

Hufanya somo kueleweka haraka; kutokana na kwa wanafunzi kujifunza kwa vitendo huweza kuelewa haraka na kukumbuka kumbukumbu kwa muda mrefu.
Na hivyo kufanya somo kwenda haraka.

**Kielelezo Na. 16.1:** *Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 16.*

Katika Kielelezo Na. 16.1, mtahiniwa aliweza kuonesha kwa usahihi umuhimu wa mbinu ya ziara katika kufundishia mada ndogo ya "Matengenezo ya baiskeli".

Aidha, watahiniwa 1,366 (34.5%) walipata ufaulu wa wastani katika swali hili kutokana na sababu mbalimbali. Baadhi yao waliweza kueleza hoja sahihi tatu hadi nne badala ya sita zilizotakiwa kwenye swali. Wengine hawakutoa maelezo sahihi au walitoa maelezo yasiyotosheleza kutetea baadhi ya hoja walizotaja. Vilevile, watahiniwa wengine walirudia hoja

zenye maana au ufafanuzi sawa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika, *mbinu ya ziara huwasaidia wanafunzi kupata taarifa ya kwanza kuhusu dhana iliyokusudiwa* na *huwasaidia wanafunzi hupata taarifa ya moja kwa moja kutoka kwa mwenyeji wao ambaye ni fundi wa baiskeli* kama hoja mbili tofauti wakati kimsingi hoja ya pili ni ufafanuzi wa hoja ya kwanza.

Pamoja na ufaulu mzuri katika swali hili, watahiniwa wachache (0.1%) walipata ufaulu hafifu kutokana na sababu mbalimbali. Baadhi yao walionesha kukosa maarifa kuhusu dhana ya mbinu za kufundishia somo la Stadi za Kazi, hivyo waliandika hoja zisizo sahaihi kama vile: *huwasaidia wanafunzi kutengeneza vitu mbalimbali, humsaidia mwanafunzi kujifunza mada nyingi kwa wakati mmoja, huwafanya wanafunzi kuhusisha mambo wanayojifunza kwenye ziara na maisha yao ya kila siku, huupima usikivu wa wanafunzi, humfanya mwanafunzi ajione ni mtu muhimu* na *hukuza stadi ya mawasiliano*. Watahiniwa wengine walishindwa kuelewa matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika mbinu mbalimbali za kufundishia ambapo alitaja: *mbinu ya kualika mgeni, onyesho mbinu, mbinu ya majadiliano, kazi mradi* na *mhadhara*. Mtahiniwa mwingine aliandika, *gereji bubu za baiskeli, gereji, kiwandani* na *duka la baiskeli na vifaa vya baiskeli*. Mtahiniwa huyu alishindwa kuelewa kuwa haya ni maeneo ambako wanafunzi wanaweza kwenda kwa ajili ya kujifunza mada ndogo ya *Matengenezo ya baiskeli* na sio umuhimu wa mbinu ya ziara katika kufundishia mada hiyo. Hali kadhalika, watahiniwa wengi katika kundi hili hawakuweza kuandika utangulizi na hitimisho linaloendana na dhana iliyopimwa kwa kuwa hawakuwa na stadi ya uandishi wa insha.

## 3.0 UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA KUFAULU KWA WATAHINIWA KATIKA MADA

Mtihani wa somo la Stadi za Kazi kwa mwaka 2019 ulikuwa na maswali 16 yaliyotungwa kutoka katika mada 11. Kiwango cha kufaulu kilikuwa kizuri kwani kwa wastani, asilimia 76.4 ya watahiniwa walipata alama 40 na zaidi katika mtihani huu. Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa umeonesha kuwa mada 7 zilikuwa na kiwango kizuri cha kufaulu, mada 3 zilikuwa na kiwango cha wastani na mada 1 ilikuwa na kiwango hafifu (dhaifu). Rejea Kiambatisho A.

Mada zilizokuwa na kiwango kizuri cha kufaulu na kiwango chake cha kufaulu kwenye mabano ni: *Kilimo, ufugaji na uvuvi (100%), Upishi*

*(99.1%), Misingi ya kufundishia somo la Stadi za Kazi (97.7%), Ususi (97.3%), Upimaji (94.2%), Ufundishaji (92.0%)* na *Ushoni wa nguo (82.0%)*. Ufaulu wa kiwango kizuri katika mada hizi umetokana na sababu mbalimbali, kama vile: watahiniwa wengi kuwa na ujuzi na maarifa ya kutosha kuhusu mada hizi, uelewa mzuri wa matakwa ya maswali na uelewa kuhusu uandishi wa insha. Kwa hiyo, watahiniwa walitumia maarifa, ujuzi na mbinu sahihi ili kuweza kujibu maswali kwa usahihi. Mada za *Sanaa za maonyesho (63.3%), Maandalizi ya ufundishaji (50.6%)* na *Usanii wa picha, chapa, maumbo na mapambo (49.0%)* zilikuwa na kiwango cha kufaulu cha wastani. Mada pekee iliyokuwa na kiwango hafifu cha kufaulu ni ya *Muziki (14.8%)*. Ukosefu wa maarifa ya kutosha na kushindwa kuelewa matakwa ya swali ni kati ya sababu za ufaulu hafifu katika mada hii.

Ulinganifu wa kufaulu kwa watahiniwa katika mada kwa mwaka 2018 na 2019 umeonesha kuwa kiwango cha kufaulu kimepanda kutoka kiwango cha wastani kwenda kiwango kizuri katika mada ya *Kilimo, ufugaji na uvuvi*. Ufaulu ulishuka toka kiwango kizuri kwenda kiwango cha wastani katika mada za *Maandalizi ya ufundishaji, Usanii wa picha, chapa, maumbo na mapambo* na *Sanaa za maonyesho.* Aidha, mada za *Ususi, Ushoni wa nguo, Upishi, Upimaji, Ufundishaji* na *Misingi ya kufundishia somo la Stadi za Kazi* zimeendelea kuwa na kiwango kizuri cha kufaulu wakati mada ya *Muziki* imekuwa ni mada pekee ambayo imeendelea kuwa na kiwango hafifu cha kufaulu. Rejea Kiambatisho B.

## 4.0 HITIMISHO

Kwa ujumla, kiwango cha kufaulu kwa mwaka 2019 kilikuwa kizuri kwa kuwa asilimia 99.98 ya watahiniwa waliofanya mtihani huu walifaulu. Aidha, uchambuzi uliofanywa katika majibu ya watahiniwa umeonesha kuwa watahiniwa wachache walishindwa kufanya vizuri katika baadhi ya maswali kutokana na sababu mbalimbali, kama vile: kushindwa kuelewa matakwa ya maswali, kukosa maarifa ya kutosha kuhusu dhana mbalimbali zilizopimwa na uelewa mdogo katika kujibu maswali ya insha. Hali kadhalika, watahiniwa hao walishindwa kutoa maelezo ya kutosha katika kutetea hoja za kujibu maswali, hali ambayo iliathiri kiwango cha kufaulu kwao katika baadhi ya maswali.

Taarifa hii ya uchambuzi itasaidia kuinua zaidi kiwango cha kufaulu katika somo la Stadi za Kazi. Hii ni kwa sababu itatoa mwongozo kwa wakufunzi

na wawezeshaji katika ufundishaji wa mada zilizoonekana kuwa na ufaulu hafifu na wastani. Itatoa pia dira kwa walimu tarajali na kuwahamasisha katika ujifunzaji wa mada zote za somo la Stadi za Kazi ili kuwapa uwezo wa kufahamu vizuri fani mbalimbali zinazofundishwa kwenye somo hilo.

Aidha, taarifa hii ya uchambuzi itakuwa na tija kwa wakufunzi katika ufundishaji, utungaji na usahihishaji wa mazoezi, majaribio na mitihani, hususani katika kuinua kiwango cha kufaulu katika somo la Stadi za Kazi. Taarifa hii pia inatarajiwa kutoa hamasa kwa walimu tarajali kuzielewa vizuri fani zinazofundishwa kwenye somo la Stadi za Kazi ili kuwapatia stadi muhimu za maisha.

Mwisho, taarifa hii ya uchambuzi wa ufaulu kwa watahiniwa itakuwa dira itakayowasaidia wakufunzi na walimu tarajali kuzielewa changamoto zilizosababisha watahiniwa wachache kutojibu vizuri baadhi ya maswali na kisha kuzirekebisha.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Kutokana na uchambuzi wa majibu ya watahiniwa, mapendekezo yafuatayo yalitolewa ili kuinua kiwango cha kufaulu katika somo hili:

(a) Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa Elimu iandae warsha na mafunzo kazini ili kuwajengea wakufunzi uwezo wa kufundisha fani zote za somo la Stadi za Kazi kwani sio wakufunzi wote ni wataalamu wa fani za somo hili.

(b) Wadau wa elimu wahimizwe kuandika vitabu vya kiada na ziada na majarida ya somo la Stadi la Kazi ili kuwajengea wanachuo maarifa na umahiri na kuwapa pia uelewa wa pamoja katika stadi zinazofundishwa katika somo hili.

(c) Wakufunzi watoe mazoezi, majaribio na mitihani ya kutosha, kusahihisha, kutoa mrejesho na kufanya masahihisho ili kuwajengea wanachuo uwezo wa kujibu vizuri maswali ya mtihani wa Taifa.

(d) Wakufunzi wafundishe mada zote zilizoainishwa katika muhtasari ili kutoa maarifa na uwezo kwa wanachuo kujibu maswali kwa usahihi katika mtihani. Hii itasaidia pia kuleta uwiano mzuri wa ufaulu katika mada zote za somo hili.

(e) Mbinu shirikishi zitumike katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Stadi za Kazi ili kuwajengea walimu tarajali uwezo wa kufikiri kwa kina, kuwa wadadisi na kugundua.

(f) Walimu tarajali washauriwe kusoma vizuri maswali na kuelewa matakwa yake kabla ya kuanza kuandika majibu.

*Kiambatisho A*

**UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA MADA**

| Na. | Mada | Namba ya Swali | Asilimia ya Ufaulu | | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Waliopata asilimia 40 na zaidi | Wastani | |
| 1 | Kilimo, ufugaji na uvuvi | 13 | 100 | 100 | Vizuri |
| 2 | Upishi | 7 | 99.1 | 99.1 | Vizuri |
| 3 | Misingi ya kufundishia somo la Stadi za Kazi | 14 | 97.7 | 97.7 | Vizuri |
| 4 | Ususi | 3 | 97.3 | 97.3 | Vizuri |
| 5 | Upimaji | 2 | 99.6 | 94.2 | Vizuri |
| | | 15 | 88.7 | | |
| 6 | Ufundishaji | 10 | 98.4 | 92.0 | Vizuri |
| | | 6 | 93.6 | | |
| | | 8 | 84.1 | | |
| 7 | Ushoni wa nguo | 12 | 82.0 | 82.0 | Vizuri |
| 8 | Sanaa za maonyesho | 11 | 63.3 | 63.3 | Wastani |
| 9 | Maandalizi ya ufundishaji | 16 | 99.9 | 50.6 | Wastani |
| | | 4 | 1.3 | | |
| 10 | Usanii wa picha, chapa, maumbo na mapambo | 9 | 97.6 | 49.0 | Wastani |
| | | 1 | 0.3 | | |
| 11 | Muziki | 5 | 14.7 | 14.7 | Daifu |
| | | | | 839.9 | |

*Kiambatisho B*

**ULINGANIFU WA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA MADA KWA MWAKA 2018 NA 2019**

| Na. | Mada | 2018 | | | 2019 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Idadi ya Maswali | Asilimia ya Waliopata asilimia 40 na zaidi | Maoni | Idadi ya Maswali | Asilimia ya Waliopata asilimia 40 na zaidi | Maoni |
| 1 | Ususi | 1 | 99.8 | Vizuri | 1 | 97.3 | Vizuri |
| 2 | Ushoni wa nguo | 1 | 99.5 | Vizuri | 1 | 82.0 | Vizuri |
| 3 | Upishi | 1 | 99.1 | Vizuri | 1 | 99.1 | Vizuri |
| 4 | Maandalizi ya ufundishaji | 1 | 98.7 | Vizuri | 2 | 50.6 | Wastani |
| 5 | Usanii wa picha, chapa maumbo na mapambo | 2 | 97.3 | Vizuri | 2 | 49.0 | Wastani |
| 6 | Upimaji | 1 | 96.8 | Vizuri | 2 | 94.2 | Vizuri |
| 7 | Ufundishaji | 4 | 92.1 | Vizuri | 3 | 92.0 | Vizuri |
| 8 | Sanaa za maonyesho | 1 | 81.7 | Vizuri | 1 | 63.3 | Wastani |
| 9 | Misingi ya kufundisha somo la Stadi za Kazi | 2 | 76.4 | Vizuri | 1 | 97.7 | Vizuri |
| 10 | Kilimo, ufugaji na uvuvi | 1 | 65.7 | Wastani | 1 | 100 | Vizuri |
| 11 | Muziki | 1 | 18.2 | Dhaifu | 1 | 14.7 | Daifu |